


Jumanne Oktoba 17, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581466
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital
epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Gia mpya maduka kubadilisha fedha nchini



• **BoT** yaja na kanuni mpya kwa wawekezaji... *Endelea ukurasa 3*



## YALIYOMO

UKURASA WA 19

### UN: MZOZO WA ISRAEL NA HAMAS WAFIKIA PABAYA

UMOJA wa Mataifa (UN) umesema mzozo kati ya Israel na Hamas umefikia hatua mbaya wakati hospitali...

UKURASA WA 19

### UGANDA, DRC ZAKUBALIANA KUSAFIRI BILA VISA

TAIFA la Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) zimekubaliana kuondoa masharti ya visa ili...

UCHAGUZI UJAO

## Samia atoa angalizo staili ya kuamua

UKURASA 2

## Mbaroni tuhuma kuzika mfanyabiashara akiwa hai

UKURASA 2

**MICHEZO** GAMONDI AWAGEUKIA KINA BACCA, MWAMNYETO UK.24

**KATUNI** UK.6




Naibu Spika, Musa Azzan Zungu, akizungumza wakati wa hafla ya utiaji saini ushirikiano wa kutoa mafunzo ya uanagenzi (mafunzo kwa vitendo) baina ya Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) na Wakala wa Vipimo (WMA), jana chuoni hapo. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

KUELEKEA UCHAGUZI

# Samia atoa angalizo staili ya kuamua

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

RAIS Samia Suluhu Hassan ametoa angalizo kwa wananchi kuwa kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024 na Uchaguzi Mkuu 2025, wasifanye kosa katika kuchagua viongozi.

Amewataka wahakikishe wanachagua watu watakaowatumikia na si kuweka watu watakaopitisha watu wengine.

Alitoa angalizo hilo jana alipozungumza na wananchi wa Wilaya ya Mkalama katika siku ya pili ya ziara yake mkoani Singida baada ya kuzindua Daraja la Msingi lililojenga katika Kijiji cha Msingi wilayani hapa kwa gharama ya Sh. bilioni 11.1.

"Tunaelekea kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa niwaombe tuendelee kutunza amani na utulivu ndani ya nchi na pia kuweka watakaowatumikia, msiende kuweka watu watakaopitisha watu wengine," alionya.

Rais Samia pia alionya kuwa katika kipindi hicho cha uchaguzi wananchi wanapaswa kujiepusha na makundi ambayo yanaweza kubomoa chama na kuzorotesha maendeleo kutokana na chuki zinazoweza kujengwa na watu walioshindwa kwenye uchaguzi.

"Ninajua kwenye uchaguzi pia kuna mkono wa Mungu, unapokosa ukatengeneza makundi unaanza kubomoa chama chetu na kufanya maendeleo yakwame kwa kuanza kutengeneza chuki, hapana! Huko tusifike," alionya.

Akizungumzia sekta ya elimu, Rais alisema kwa sasa changamoto iliyopo ni ukosefu wa nyumba za kuishi walimu. Serikali katika bajeti ya mwakani itatenga fedha za kutosha kwa ajili ya kujenga nyumba hizo ili walimu wapate sehemu za kuishi na hivyo kufundisha vizuri.



Rais Samia alisema baadhi ya changamoto zilizopo katika sekta ya elimu kama vile ujenzi wa vyoo zinaweza kutatuliwa na halmashauri katika maeneo husika badala ya kusubiri serikali kuu kutoa fedha.

Alisema Wilaya ya Mkalama ambayo ina miaka 11 tangu kuanzishwa kwake, viongozi wake wasibweteke kwa uchanga wa wilaya na badala yake waongeze jitihada ili wilaya ikue zaidi kimaendeleo.

Aliongeza kuwa serikali inatambua tatizo la upungufu wa watumishi katika sekta ya elimu hususani walimu na hivyo inaendelea kulipatia ufumbuzi suala hilo. Wilaya ya Mkalama ina upungufu wa walimu wa shule za msingi kwa asilimia 40 na wa sekondari asilimia 26.

Kuhusu bajeti ndogo inayotolewa kwa Wilaya ya Mkalama, Rais Samia alimwagiza Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa, kushughulikia tatizo hilo.

Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa alisema Daraja la Msingi ni kiunganishi muhimu kwa mikoa ya Simiyu na Mara kutoka Mkoa wa Singida, hivyo limewekwa taa ili kuling'arisha nyakati za usiku.

**AONYA WANANCHI**

Katika hatua nyingine, Rais Samia ameonya wananchi kuhusu tabia ya kujichukulia sheria mikononi, badala yake kunapotokea matukio katika maeneo yao wayapeleke vituo vya polisi ili taratibu za kisheria zichukuliwe.

Alitoa onyo hilo jana alipozungumza na wananchi wa Ikungi baada ya kuzindua vituo vya polisi vya kisasa vya Wilaya za Ikungi na Mkalama mkoani Singida ambavyo vimejengwa kwa zaidi ya Sh. bilioni mbili.

"Baada ya serikali kujenga vituo hivi vya polisi, sasa mambo ya kujichukulia sheria mikononi yaishe na wale wahalifu hapa patakuwa nyumbani kwao," alisema.

Rais Samia pia aliwataka maofisa wa Jeshi la Polisi kutoa huduma nzuri kwa wananchi kwa kuwa suala la kuwa na jengo ni jambo moja na kutoa huduma bora ni jambo lingine.

Awali, Mkadiriaji Majengo wa Jeshi la Polisi, Aisha Tuwa, alimweleza Rais kuwa Kituo cha Polisi Wilaya ya Ikungi kimejengwa katika eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 4,046 na jengo hilo lina vyumba vinane na sakafu ya chini ina mita za mraba 889.

Alisema ndani ya jengo hilo mna vyumba vya mahabusu vitano, chumba cha mahabusu watoto wa kike kimoja, chumba cha mahabusu watoto wa kiume, chumba cha mahabusu cha wanaume, chumba cha mahabusu wanawake na chumba cha mahabusu cha watu wenye mahitaji maalum.

Tuwa alisema ndani ya jengo hilo pia mna chumba cha mashtaka na chumba cha Ofisi ya Mkuu wa Kituo wakati katika sakafu ya juu kuna vyumba 12 ikiwamo chumba cha Mkuu wa Polisi wa Wilaya, Mkuu wa Upelelezi Wilaya, ukumbi wa mikutano na nyumba za makazi ya askari sita.

Akihutubia wananchi katika Uwanja wa People's Bombardier mjini Singida katika maadhimisho ya miaka 60 ya Mkoa wa Singida, Rais Samia aliwataka wananchi kutumia fursa za rasilimali za asili walizonazo kama vile jiografia, madini na misitu kwa ajili ya maendeleo.

Alisema inasikitisha kuona ndani ya miaka 60 ya mkoa huo unachangia asilimia mbili pekee katika Pato la Taifa, licha ya kuwa ni kati ya mikoa mitano ya mwisho kwa umaskini nchini na una rasilimali za asili za kutosha.

Kwa mujibu wa Rais Samia, mkoa huo una jumla ya hekta 26,893 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na kuwataka watumie fursa hiyo katika kukuza kilimo, kutokana na kukabiliwa na changamoto ya kuwa na kiwango kidogo cha mvua.

Aliwaelekeza viongozi wa mkoa huo kuhamasisha wananchi kupanda mazao yanayostahamili ukame na kutumia mbegu bora na za muda mfupi kama alizeti, ufuta, dengu na korosho pamoja na ufugaji wa nyuki.

"Tuna madini mengi Singida, sasa wanapokuja wawekezaji tusiwe kama 'majoka ya mdimu', tuwapishe watumie hayo maeneo wajenge Singida wapate faida yao waliokuja kuitafuta.

"Kwa upande wetu serikali kuu tutaendelea kuunga mkono vipaumbele vya maendeleo ya mkoa kwa kuweka mazingira wezeshi."

## Mfanyabiashara auawa kisha azikwa akiwa hai

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

JESHI la Polisi mkoani Rukwa linawashikilia watu watatu wakazi wa Kijiji cha Katazi, wilayani Kalambo kwa tuhuma za kumpiga rungu mfanyabiashara wa mazao, Baraka Nyangala (30), kisha kumzika akiwa hai.

Imedaiwa, watuhumiwa hao walikuwa na lengo la kupora fedha alizokuwa amebeba mfanyabiashara huyo kwa ajili ya kununua mazao.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rukwa, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP), Shadrack Masija, tukio hilo lilitokea jana wakati mfanyabiashara huyo alipokwenda kununua maharage akiwa na watu wanaotuhumiwa kumfanyia unyama huo.

Ilidawa kuwa mfanyabiashara huyo alipigiwa simu na watuhumiwa, Frank Simsokwe (33), Edfonsi Simsokwe (28) ambao ni ndugu na Nikas Lunguya (38) kuwa wana maharage na kumtaka akayaangalie kamaataridhika nayo ayanunue.

Taarifa zilidai, alipofika kijijini hapo wakatumia usafiri wake wa pikipiki kumpeleka sehemu yalipo maharage hayo na walipofika porini walimtaka mfanyabiashara huyo asimamishe pikipiki yake.

"Baada ya kusimamisha pikipiki hiyo mmoja kati ya watuhumiwa hao alimpiga kwa rungu kichwani mfanyabiashara huyo ambaye alipoteza fahamu kisha wakampora fedha taslimu Sh. 1, 840,000 na pikipiki," alisema Kamanda Masija.

Kamanda alisema, baada ya kumjeruhi kichwani na kuona amepoteza fahamu waliamua kuchimba shimo kisha kumfukia akiwa bado hai na kutokomea kusikojulikana.

Alisema baada ya ndugu wa mfanyabiashara huyo kutomwona ndugu yao, walitoa taarifa polisi ambao kwa kutumia intelijensia na wataalamu wa Cyber-crime waliwakamata watu hao.

ACP Masija alisema watuhumiwa hao waliwaongoza hadi eneo walilomfukia na alipofukuliwa alikuwa ameshafariki kwa kukosa hewa. Mwili wake umekabidhiwa kwa ndugu baada ya uchunguzi.

Kamanda alisema polisi inawashikilia watuhumiwa hao na watafikishwa mahakamani baada ya uchunguzi kukamilika.

**Imedaiwa, watuhumiwa hao walikuwa na lengo la kupora fedha alizokuwa amebeba mfanyabiashara huyo kwa ajili ya kununua mazao.**

## TIB yajivunia kuwezesha ajira 30,000 nchini

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Maendeleo Tanzania (TIB) inatarajia kuongeza ajira zaidi ya 30,000 katika miradi ya sekta za kilimo, maji na nishati nchini kutokana na uwekezaji wa benki hiyo.

Mpango huo ulitangazwa jana na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TIB, Lillian Mbassy, wakati akizungumza na waandishi na wahariri wa vyombo vya habari nchini kuhusu mpango wa benki hiyo kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2022 hadi 2024.

Mbassy alifafanua kuwa TIB imewezesha wafanyakazi 30,000 kuajiriwa hadi sasa katika sekta hizo, kati ya hao, 10,000 ni wa kilimo.

Awali Mbassy alifafanua kuwa TIB imekuwa ikitoa mitaji ya muda mrefu na ya kati kwa ajili ya kuendesha miradi ya maendeleo na mingine ya dirisha maalumu lililopo katika benki hiyo.

"Tofauti na benki nyingine, TIB tumekuwa tukitoa mikopo ya muda mrefu katika sekta hizo tofauti na nyingine ambazo zimekuwa zikikopesha wateja wake kwa kipindi maalumu," alisema na kufafanua kuwa:

"Mfano mkopo unaotolewa kwa kilimo, mkopaji anaweza kulipa wakati wa msimu wa mavuno baada ya kuuza mazao yake."

Aliyataja malengo mengine ya TIB kuwa ni kuongoza mapato ya serikali kupitia kodi na tozo zinatozwa kwa kampuni hizo, kuhakikisha upatikanaji wa majisafi na salama katika jamii na kuboresha afya, kusimamia fedha na wakala.

Hadi mwezi Septemba, mwaka huu, TIB ilikuwa imefanya uwekezaji wa Sh. bilioni 988.7 katika miradi ya muda mrefu inayotekelezwa na serikali na sekta binafsi nchini.

Kwa upande wa sekta ya kilimo, imewekeza kwenye miradi 253 iliyopo wilaya 76 na mikoa 23 nchini na kutoa ajira kwa wafanyakazi 10,000.

Kadhalika, katika miaka miwili, serikali imefanya uwekezaji mkubwa katika sekta ya maji kwa fedha zinazotolewa na TIB na kwamba Benki ya Dunia (WB) wamekuwa wakienda kubadili pampu zinazotumia dizeli na kuweka umeme wa jua na kunufaisha zaidi ya jumuiya 60.

Alisema, TIB pia inatoa huduma ya usimamizi wa mifuko kwa niaba ya serikali na wadau wengine.

Kwa fedha zake, TIB imewekeza Sh. bilioni 12.3 kwa taasisi kubwa kama TANESCO kwa ajili ya nishati mwegawati 8.84 za umeme zimezalishwa na kuingizwa katika gridi ya taifa.

Benki hiyo pia inatoa mitaji kwa taasisi zote nchini ili kuhakikisha miradi inayotekelezwa ina kuwa chanya kwa manufaa ya jamii na kukuza uchumi wa taifa.

Alisema lengo la kuanzishwa kwa TIB ni kujenga Tanzania ya maendeleo ya kiuchumi.

TIB ni taasisi ya 19 chini ya Ofisi ya Msajili wa Hazina ambazo zimefanya kikao kazi na waandishi, wahariri kuelezea umma majukumu yao kama ilivyoagizwa na Mkurugenzi, Nehemia Mchechu.

Mchechu aliagiza taasisi zilizopo chini ya ofisi yake kukutana na waandishi na wahariri kuulezea umma utekelezaji wa majukumu yao, mafanikio na matarajio yao ili wananchi waweze kufahamu majukumu yao.



Waombolezaji wakibeba jeneza lenye mwili wa aliyekuwa mtangazaji wa kituo cha televisheni cha ITV, Shabani Tole, katika makaburi ya Kisutu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Gia mpya maduka ya kubadilisha fedha

**Na Maulid Mmbaga**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imetoa kanuni mpya za maduka ya kubadilisha fedha za kigeni nchini ambazo zimegawanyika katika madaraja matatu ya leseni, huku kiwango cha juu cha mtaji wa kuanzisha duka hilo kikiwa ni Shilingi bilioni moja.

Kanuni za sasa zimetoa ahueni kwenye mtaji kwa wenyeji, huku zikipunguza ada ya leseni kwa mwaka kutoka Sh. milioni moja hadi 500,000, na ada ya maombi ikibaki iliyokuwapo ya Shilingi milioni moja katika kanuni za mwaka 2019.

Aidha, kanuni za sasa zipo katika lugha zote mbili yaani Kiswahili na Kiingereza, wakati za mwaka 2019 zilikuwa kwa lugha ya Kiingereza pekee.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa jana na Gavana wa BoT, Emmanuel Tutuba, duka la kubadilisha fedha za kigeni daraja A, litakalomilikiwa na mgeni au mwenyeji litaruhusiwa kufungua matawi sehemu yoyote ndani ya Tanzania.

Alisema kwa duka daraja A linalomilikiwa na wageni litatakiwa kuwa na mtaji usiopungua Shilingi bilioni moja na linalomilikiwa na mwenyeji litatakiwa kuwa na mtaji usiopungua Sh. milioni 500, ikiwa ni ahueni kwa kuwa kanuni za mwaka 2019 kiwango cha mtaji kilikuwa kimoja.

"Duka daraja A litaruhusiwa kufanya miamala ya papo kwa papo, kutuma fedha na kufanya biashara kama wakala wa benki, taasisi ya fedha, kampuni ya bima, mtoa huduma wa fedha kwa njia ya simu, au huduma nyingine zozote za fedha kama itakavyoidhinishwa na BoT," alisema Tutuba.

Kadhalika duka la kubadilisha fedha za kigeni daraja B ni linalomilikiwa na wenyeji ambalo halitaruhusiwa kufungua matawi kwa ajili ya kufanya biashara ya kubadilisha fedha za kigeni. Pia litatakiwa kuwa na mtaji usiopungua Sh. milioni 200.

Tutuba alifafanua kuwa kanuni nyingine ya duka daraja B, litaruhusiwa kufanya miamala ya papo kwa papo na kufanya biashara kama wakala wa benki, taasisi ya fedha, kampuni ya bima, mtoa huduma wa fedha kwa njia ya simu, au huduma nyingine zozote za fedha kama itakavyoidhinishwa na BoT.

"Mtu anayekusudia kuendesha duka la kubadilisha fedha za kigeni Daraja A au B atatakiwa kuomba leseni kwa kuandika barua benki na maombi hayo yatasainiwa na mkurugenzi," alisema na kuongeza:

"Kama ni kampuni, majina ya wakurugenzi wasiopungua wawili, au mtu aliyeidhinishwa na mwombaji yataambatanishwa na nakala iliyothibitishwa ya azimio la bodi linaloidhinisha maombi, fomu A iliyoainishwa katika jedwali ikiwa imejazwa kikamilifu, nakala iliyothibitishwa ya cheti cha usajili na ya katiba na kanuni za kampuni," alisema Tutuba.

Aidha, kanuni za duka daraja C, alibainisha kwamba ni lililoanzishwa na hoteli yenye hadhi ya nyota tatu au zaidi kwa ajili ya kufanya miamala ya papo kwa papo kwa wateja wa hoteli pekee.

Vile vile, alisema leseni ya duka daraja C itatolewa kwa hoteli au mmiliki wa hoteli, na halitatakiwa kuwa na mtaji wa kufanyabiashara ya kubadilisha fedha za kigeni.

Pia alisema mwombaji wa leseni ya duka la kubadilisha fedha za kigeni daraja A au B atatakiwa ndani ya miezi sita baada ya kupewa idhini ya awali, kuwasilisha benki, taarifa ya akaunti ya benki yenye jina la duka la kubadilisha fedha za kigeni inayothibitisha kiasi kilichotengwa kama mtaji uliolipwa kwa fedha za Tanzania au kigeni.

Kanuni za sasa zimeweka masharti kuwa duka la kubadilisha fedha za kigeni Daraja A na B litalipa ada ya mwaka ya Sh. 500,000 kwa kila tawi linaloendesha biashara, na mabadiliko yoyote ya umiliki wa duka yatahitaji kupata idhini ya benki kabla ya kufanyika.

Mengine ni uthibitisho wa malipo ya ada ya maombi ya leseni isiyorejeshwa ya Shilingi milioni moja, nakala iliyothibitishwa ya mkataba wa upangishaji au hatimiliki yenye jina la mwombaji, na ushahidi kwamba eneo la biashara limewekwa kamera za usalama (CCTV) katika maeneo yote ya kimkakati, ikiwa ni pamoja na kaunta au vizimba vya kutolea huduma na sehemu za kupumzikia wateja.

Pia zinataka taratibu za kimaandishi zinazoainisha namna ya kugundua na kutoa taarifa za matukio ya utakatishaji fedha kwa kuzingatia sheria na kanuni za kuzuia utakatishaji wa fedha haramu na upambanaji wa ufadhili wa ugaidi.

Nyingine mwombaji wa leseni ya duka daraja A anayekusudia kutoa huduma ya kutuma fedha atatakiwa, pamoja na taarifa zinazohitajika chini ya kanuni ndogo ya kuwasilisha benki ushahidi kwamba akaunti maalum itakayotumika mahsusi kwa lengo la kuweka fedha ya mteja ikisubiri kutumwa au kupokelewa, imefunguliwa katika benki au taasisi ya fedha.

"Pia atatakiwa kuwasilisha ushahidi kwamba amana isiyozaa riba ya Dola za Marekani 100,000 imewekwa benki kwa ajili ya duka la kubadilisha fedha za kigeni daraja A lenye umiliki wa hisa zaidi zinazomilikiwa na wageni na dola 50,000 kwa ajili ya duka daraja A lenye umiliki wa hisa zaidi zinazomilikiwa na wenyeji," ilisema sehemu ya kanuni hizo.

Alieleza kuwa duka la kubadilisha fedha za kigeni halitatakiwa kuanza biashara mpaka pale, eneo la biashara, mitambo ya usalama, mawasiliano, vifaa vya uchakataji, na mifumo ya hesabu za fedha iwe imewekwa, imekaguliwa, imepitiwa na kuidhinishwa na Benki.

MAZUNGUMZO MAALUMU -4

# Kimiti akumbuka alivyompatia Nyerere dola 20,000 Uholanzi

Na Mwandishi Wetu

**"MWAKA Mwalimu Julius Nyerere (Rais wa Kwanza wa Tanzania) alitembelea Uholanzi na tukakutana naye na kuzungumza naye akatueleza mambo yanavyoendelea nchini. Nasi vijana wa Tanzania tuliokuwa tunasoma huko wakati ule, tuliona tufanye jambo. Tukaona tumpatie Dola za Marekani 20,000."**



Hiyo ni simulizi ya mwanasiasa mkongwe, Paul Kimiti, ambaye katika maisha yake ya utumishi wa umma na siasa aliwahi kushika nyadhifa mbalimbali kabla hajastaafu. Alisimulia hayo alipozungumza na Nipashe hivi karibuni, nyumbani kwake, Dar es Salaam.

Anasema Mwalimu Nyerere alishangaa vijana waliopelekwa na serikali kusoma wanatoa fedha kwa serikali. Kimiti anasema waliamua kufanya hivyo ikiwa ishara ya kulipa fadhila kwa serikali.

"Tuliona tufanye hivyo nami nilimwambia Mwalimu kwamba tumeona serikali imetulipia kila kitu na mimi mtoto wa dereva ningefikaje huku kama siyo serikali? Tulionyesha shukrani zetu kwa serikali kwa kutuchagua sisi wachache kati ya vijana wengi wa Tanzania kwenda nje kusoma. Tuliona tufanye hivyo," anasema.

Pamoja na kupelekwa Uholanzi kusomea shahada ya kilimo, Kimiti anasema aliwashawishi Watanzania wenzake kwamba pamoja na kusoma watafute kazi ili kujipatia kipato na sehemu ya fedha watakazopata wapeleke nyumbani. Hivyo ndivyo walivyofanya na kupata kiasi ambacho walimkabidhi Nyerere.

Wakati wanasoma, anasema walikuwa wakilipwa mishahara, ada na kila kitu, hivyo waliona wafanye kazi pia ili fedha wanayopata kupitia kazi, watume nyumbani kusaidia wazazi, ndugu na jamaa zao.

**ALIANZISHA BENDI**

Katika kutimiza azma hiyo, Kimiti alianzisha bendi ya muziki iliyojulikana kama Safari Brothers akiwa na Mtanzania mwenzake, Alphonce Joseph Lyimo, kutoka Marangu mkoani Kilimanjaro, ambaye kwa sasa ni marehemu.

"Tukiwa na bendi hii, tulipata mafanikio makubwa. Tulisaidiwa na kampuni ya Philips, hii ni kampuni maarufu iliyokuwa inatengeneza redio, mafriji na betri. Ni kampuni ambayo ilikuwa haiwezi kukubali kama mtu hana wimbo mzuri kuurekodi. Kutokana na kazi yetu kuwa nzuri, Philips ilikubali kurekodi nyimbo zetu," anabainisha.

Kimiti pia anafichua kwamba mwenzake Lyimo alioa mwanamke Mholanzi ambaye anasema mpaka sasa bado yuko hai na yuko Marangu.

"Binafsi sikutaka kuoa mzungu kwa sababu baba alisema kama nitaoa mzungu basi nibaki huko huko na kweli niliona nitampelekaje mzungu kule kwetu Sumbawanga?" Anasema.

Licha ya kutokuoa huko, anasema alikuwa na mpango wa kutorejea Tanzania lakini alisalimu amri baada ya serikali kuonya kuwa yeyote ambaye hatarudi nyumbani baada ya kumaliza masomo, atanyang'anywa pasipoti.

**KAZI NA AJIRA**

Safari ya maisha ya kazi na ajira kwa Kimiti vinaanzia mwaka 1959 baada ya kumaliza kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Mzumbe mkoani Morogoro. Anasema alipangiwa kozi ya masuala ya posta na simu Nairobi, Kenya lakini alikataa na kuomba ajira kilimo.

"Katika kipindi kile baada ya kumaliza elimu, ulikuwa huwezi kupata nafasi ya kwenda chuoni hivyo lazima ufanye kazi kwanza. Ulikuwa lazima uende kijijini ukafanye kazi kwa miaka miwili na baada ya hapo, wakiridhika ndipo unapewa nafasi ya kujiunga na chuo.

> "Ikulu iliingilia kati nirudishwe Uyole lakini baadaye mwaka 1979 nilihamishwa kwenda Chuo cha Kilimo Nyegezi (sasa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino-SAUT). Nilikaa pale hadi mwaka 1980 nilipoomba kwenda Sumbawanga kuomba ubunge kupitia Viti vya Taifa.

"Baada ya hapo nilipangwa kwenda Chuo cha Kilimo na Mifugo Tangeru, Arusha, kwa kozi ya miaka miwili. Sikumaliza kozi ile kwani nilichaguliwa kwenda Uholanzi kwa masomo ya diploma ya kilimo miaka miwili. Baada ya kumaliza niliomba kuongezewa mwaka mmoja wa elimu ya kilimo ili kufundisha wanafunzi wa kilimo," anasema huku akibainisha kuwa alikubaliwa.

Baada ya kurejea nchini mwaka 1967, Kimiti alipangiwa kufundisha katika Chuo cha Kilimo Ukiliguru, Mwanza, alikofanya kazi mpaka mwaka 1969 alipopigiwa simu na Nyerere aende makao makuu ya chama tawala cha TANU (wakati huo) kuwa mwalimu wa siasa.

"Nafasi niliyopewa ilikuwa ya Katibu wa Chama, hivyo lazima mtu awe amepitia mafunzo kuhusu chama. Nilijiuliza nitaendaje kufanya kazi bila kozi? Nikaambiwa utajifunzia humo humo," anakumbuka huku akieleza baadhi ya kazi alizofanya kuwa ni pamoja na kutoa elimu ya vipindi katika iliyokuwa Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD) vilivyokuwa vikijulikana kama SAUTI YA TANU.

Licha ya kufanya kazi hiyo, alianza kuandika vitabu vya siasa ya TANU katika kilimo ambavyo dibaji yake iliandikwa na Dereck Bryson, aliyekuwa Waziri wa Kilimo. Anaamini kwamba mchango wa vitabu hivyo, ulizaa Azimio la Iringa la mwaka 1972 la Siasa ni Kilimo. Baadhi ya vitabu hivyo, anasema vilitoa mwongozo wa uongozi bora wa vijiji, na uongozi bora kwa vijana kuanzia chipukizi.

Alifanya kazi hiyo hadi mwaka 1971 alipopata nafasi ya kusoma shahada ya uzamili katika kilimo nchini Marekani. Alisoma kozi hiyo kwa miaka miwili na kurejea nchini alipopangwa kufundisha katika Chuo cha Kilimo Uyole, Mbeya.

Katika kipindi hicho pia aliteuliwa kuwa Mkuu wa Chuo cha Kilimo Uyole wakati huo kikifadhiliwa na nchi za Scandinavia (Finland, Denmark, Norway na Sweden). Anakumbuka wakati huo chuo kilikuwa na wanafunzi 40 kutoka Ulaya na Waafrika sita tu.

Mwaka 1977 alihamishwa kwenda Naliendele mkoani Mtwara lakini anasema miezi mitatu baadaye alirejeshwa Uyole kwa kuwa ilionekana kama ameshushwa daraja kwa sababu Naliendele ilikuwa inafundisha ngazi ya cheti wakati Uyole ilikuwa Diploma.

"Ikulu iliingilia kati nirudishwe Uyole lakini baadaye mwaka 1979 nilihamishwa kwenda Chuo cha Kilimo Nyegezi (sasa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino- SAUT). Nilikaa pale hadi mwaka 1980 nilipoomba kwenda Sumbawanga kuomba ubunge kupitia Viti vya Taifa.

"Katika kinyang'anyiro kile kwa mkoa wa Rukwa tulikuwa watatu. Mimi, Profesa Athanas Kauzeni na Chama Omari Matata. Katika kura zile nilipata asilimia 90 na wenzangu wakaambulia asilimia 10. Nilichaguliwa kuwa mbunge lakini niliendelea kuwa mkuu wa chuo," anasema.

Profesa Kauzeni alikuwa mwanataaluma wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika Taasisi ya Tathmini ya Rasilimali (IRA) na aliwahi kuwa mkurugenzi wa taasisi hiyo kwa sasa ni marehemu. Matata alikuwa mtangazaji maarufu wa Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC).

**SAFARI YA SIASA**

Baada ya kuchaguliwa kuwa mbunge, mwaka 1982 Kimiti aliteuliwa kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Serikali za Mitaa na Vyama vya Ushirika, nafasi ambayo aliishika hadi mwaka 1984 alipoteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro.

Mwaka 1989 alihamishwa kutoka Kilimanjaro kwenda Kagera kwa wadhifa huo huo alikokaa hadi mwaka 1991 na kuhamishiwa Mbeya. Alikaa Mbeya hadi mwaka 1995 alipokwenda kugombea ubunge katika Jimbo la Sumbawanga Mjini. Alikaa katika nafasi hiyo kwa miaka 15 hadi mwaka 2020 alipoamua kung'atuka.

Kutokana na kushinda ubunge mwaka 1995, aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa, alimteua katika baraza lake la kwanza la mawaziri akimteua kuwa Waziri wa Kilimo. Alidumu katika nafasi hiyo hadi mwaka 1989 alipohamishiwa Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana hadi mwaka 2000.

Wakati Mkapa anapanga Baraza la Mawaziri baada ya kuchaguliwa Rais mwaka 1995, Kimiti anakumbuka baadhi ya magazeti nchini yalivyomtabiria kuwa Waziri Mkuu. Magazeti kama Mtanzania, Majira na Nipashe yaliandikwa katika kurasa za mbele kwamba 'Kimiti anukia Uwaziri Mkuu. Hata hivyo hakuipata na nafasi hiyo ilichukuliwa na Frederick Sumaye.

Baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2000, alishinda tena ubunge Sumbawanga Mjini lakini hakurejeshwa katika Baraza la Mawaziri. Katika uchaguzi mkuu wa Chama Cha Mapinduzi wa mwaka 2002, Kiliti aligombea ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) kundi la Tanzania Bara na aliibuka na ushindi wa kishindo wa kuwa kati ya watu 10 bora kwenye nafasi hiyo.

Katika Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana, Kimiti anasema moja ya majukumu lilikuwa kuwahudumia watu wenye ulemavu kundi ambalo anakiri kuwa ni gumu katika kulisimamia.

Tofauti na watangulizi wake, Balozi Ahmed Hassan Diria na Sebestian Kinyondo ambao walikumbwa na zahama ya kupigwa na watu wenye ulemavu, Kimiti anasema alishirikiana na kundi hilo kupitia vyama vyao katika kutatua changamoto zao.

"Kwenye Wizara ile kulikuwa na changamoto. Wenzangu walikumbana na rabsha kutoka kwa wenye ulemavu lakini mimi nilifanya nao vizuri mpaka wakafurahi. Wenzangu walikuwa wanataka kila kitu kiende kwa utaratibu lakini mimi niliona niwachukulie kama walivyo na tulikwenda pamoja," anasisitiza.

Mbali na nyadhifa hizo, Kimiti amewahi kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika ya Idadi ya Watu mwaka 2002, Mwenyekiti wa Chama cha Wabunge cha Idadi ya Watu na Maendeleo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Ranchi za Taifa (NARCO) hadi mwaka 2020 na Mjumbe wa Bunge la Katiba.

Kwa sasa, Kimiti ni Mwenyekiti wa Taasisi ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ambayo imesajiliwa Tanzania Bara na Visiwani. Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi hiyo ni Waziri Mkuu Mstaafu Mizengo Pinda na wajumbe ni Zakia Meghji, Pandu Ameir Kificho, Maua Abeid Daftar, Balozi Brigedia Jenerali (mstaafu) Mndolwa na Jeetu Patel.

TANGAZO

tigo pesa

# Ni Zaidi ya Pesa

## Ada za wateja. Piga *150*01#

| Kiwango (Tsh) | | Kutuma pesa kwenda Tigo Pesa | | | Kutuma pesa kwenda Mitandao washirika | | | Kutoa pesa kwa Wakala/ATM | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kuanzia | Mwisho | Ada ya Tigo Pesa | Tozo ya Serikali | Jumla ya Makato | Ada ya Tigo Pesa | Tozo ya Serikali | Jumla ya Makato | Ada ya Tigo Pesa | Tozo ya Serikali | Jumla ya Makato |
| 100 | 999 | 15 | 10 | 25 | 15 | 10 | 25 | - | 10 | 10 |
| 1,000 | 1,999 | 30 | 10 | 40 | 45 | 10 | 55 | 300 | 10 | 310 |
| 2,000 | 2,999 | 30 | 10 | 40 | 45 | 10 | 55 | 400 | 10 | 410 |
| 3,000 | 3,999 | 50 | 14 | 64 | 90 | 14 | 104 | 600 | 14 | 614 |
| 4,000 | 4,999 | 60 | 27 | 87 | 90 | 27 | 117 | 650 | 27 | 677 |
| 5,000 | 6,999 | 130 | 54 | 184 | 180 | 54 | 234 | 950 | 54 | 1,004 |
| 7,000 | 9,999 | 150 | 56 | 206 | 180 | 56 | 236 | 1,000 | 56 | 1,056 |
| 10,000 | 14,999 | 360 | 102 | 462 | 495 | 102 | 597 | 1,450 | 102 | 1,552 |
| 15,000 | 19,999 | 360 | 195 | 555 | 495 | 195 | 690 | 1,450 | 195 | 1,645 |
| 20,000 | 29,999 | 380 | 306 | 686 | 540 | 306 | 846 | 1,850 | 306 | 2,156 |
| 30,000 | 39,999 | 400 | 351 | 751 | 612 | 351 | 963 | 1,850 | 351 | 2,201 |
| 40,000 | 49,999 | 410 | 419 | 829 | 675 | 419 | 1,094 | 2,350 | 419 | 2,769 |
| 50,000 | 99,999 | 720 | 573 | 1,293 | 1,125 | 573 | 1,698 | 2,700 | 573 | 3,273 |
| 100,000 | 199,999 | 1,000 | 707 | 1,707 | 1,440 | 707 | 2,147 | 3,650 | 707 | 4,357 |
| 200,000 | 299,999 | 1,200 | 821 | 2,021 | 1,710 | 821 | 2,531 | 5,300 | 821 | 6,121 |
| 300,000 | 399,999 | 1,500 | 838 | 2,338 | 2,070 | 838 | 2,908 | 6,500 | 838 | 7,338 |
| 400,000 | 499,999 | 1,500 | 982 | 2,482 | 2,250 | 982 | 3,232 | 7,000 | 982 | 7,982 |
| 500,000 | 599,999 | 2,200 | 1,245 | 3,445 | 2,880 | 1,245 | 4,125 | 7,500 | 1,245 | 8,745 |
| 600,000 | 699,999 | 3,300 | 1,532 | 4,832 | 3,870 | 1,532 | 5,402 | 8,000 | 1,532 | 9,532 |
| 700,000 | 799,999 | 3,300 | 1,700 | 5,000 | 3,870 | 1,700 | 5,570 | 8,000 | 1,700 | 9,700 |
| 800,000 | 899,999 | 3,500 | 1,750 | 5,250 | 3,870 | 1,750 | 5,620 | 8,000 | 1,750 | 9,750 |
| 900,000 | 1,000,000 | 3,500 | 1,776 | 5,276 | 5,400 | 1,776 | 7,176 | 8,000 | 1,776 | 9,776 |
| 1,000,001 | 3,000,000 | 5,000 | 1,875 | 6,875 | 5,400 | 1,875 | 7,275 | 8,000 | 1,875 | 9,875 |
| 3,000,001 | 10,000,000 | 5,000 | 2,000 | 7,000 | 5,400 | 2,000 | 7,400 | 10,000 | 2,000 | 12,000 |

| Tukio | Kuanzia | Mwisho | Ada |
|---|---|---|---|
| Kuweka pesa | 1,000 | 5,000,000 | BURE |
| Kutuma pesa kwa mteja ambaye hana akaunti ya Tigo Pesa au akaunti ya mitandao washirika | 1,000 | 1,000,000 | Ada ya kutuma + Ada ya kutoa |
| Kutoa pesa kwa mteja ambaye hana akaunti ya Tigo Pesa au akaunti ya mitandao washirika | 1,000 | 1,000,000 | BURE |
| Kutuma pesa kwenda nchi za nje | 100 | 5,000,000 | Kulingana na kiwango |
| Malipo kwa Tigo Pesa | 500 | 5,000,000 | Kulingana na kiwango |

| Tukio | Ada |
|---|---|
| Kubadilisha namba ya siri | BURE |
| Kuangalia salio/ Taarifa ndogo | 50 |
| Kurudisha muamala uliokosea (Jihudumie) | 50 |
| **Kupata taarifa ya mwezi** | **Ada** |
| Taarifa ya Mwezi jana/Mwezi huu | BURE |
| Taarifa ya Miezi 3 | 1,000 |
| Taarifa ya Mwaka 1 | 2,000 |

Kwa vigezo na masharti ya huduma tembelea tovuti: https://www.tigo.co.tz/tigo-pesa-standard-terms-and-conditions. **Ada zote zimejumuisha kodi zote zinazohusika**
Kwa Ada za huduma nyingine tembelea **tovuti; https://www.tigo.co.tz/tigo-pesa-tariffs**

**Furahia Malipo kwa Tigo Pesa:**

LiPa KWA SIMU

**KUMBUKA:**

1. Unaweza kuweka au kupokea hadi TSh 10,000,000 kwa siku na unaweza kutoa au kutuma hadi TSh 5,000,000 kwa siku, pia unaweza kuhifadhi hadi TSh 10,000,000 kwa wakati mmoja kwenye akaunti yako ya Tigo Pesa, kama usajili wako umekamilika.
2. Onesha kitambulisho chako kabla ya kuweka au kutoa pesa kwa Wakala.
3. Hakikisha taarifa zako za usajili ni sahihi kwa kupiga *106# kisha 2 au piga huduma kwa wateja kwa maelezo zaidi.
4. Hesabu pesa zako na hakikisha salio lako la Tigo Pesa linaendana na muamala uliofanya kabla ya kuondoka kwa Wakala.
5. Kila mara unapotuma pesa, kumbuka kuhakiki namba ya mpokeaji kuepuka kukosea na usumbufu.
6. Hakikisha unahifadhi namba yako ya siri (PIN), simu yako na laini yako kwa usalama. Usimpe (PIN, Simu, laini yako) wala kumtajia mtu yoyote namba yako ya siri, iwe Wakala wa Tigo Pesa, mfanyakazi wa Tigo au mhudumu wa Tigo Huduma kwa wateja. Pia kumbuka kubadili namba yako ya siri mara kwa mara.
7. Tigo itakupigia kwa 100 Tu.
8. Kutoa taarifa yoyote dhidi ya udanganyifu Piga simu namba 100 au tuma ujumbe kwenda namba 15040 au barua pepe kwenda customercare@tigo.co.tz
9. Unaweza kupokea pesa kutoka nchi zaidi ya 200 duniani, na unaweza kutuma pesa kwenda nchi zote za Mashariki na Kusini mwa Afrika .
10. Kupata vigezo na masharti ya kutumia Tigo Pesa, tembelea duka la Tigo lililopo karibu nawe au www.tigo.co.tz

Unaweza kurudisha **muamala uliokosea**, **token ya luku**, **ku-unbar akaunti yako ya Tigo Pesa** na **kuriseti PIN**

Piga ***150*01#**
chagua **6 (Jihudumie)**
kisha chagua huduma unayotaka

tigo pesa

App yenye urahisi wa kushangaza!




**Fanya malipo ya Serikali**




Pakua kwenye

Google Play | App Store

tigo pesa

Kuwasaliana na huduma kwa wateja,
Piga **100** bure au tembelea duka lolote la Tigo!
Ada hizi ni kuanzia Oktoba 2023

tigo

www.tigo.co.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Vitambulisho vya NIDA ni muhimu vichangamkiwe

**WAKATI** Tanzania ulipoanzishwa utaratibu wa kila raia kuwa na kitambulisho kitakachomtambulisha kuwa yeye ni raia wa taifa hilo, baadhi ya watu walipuuza kuvichangamkia wakati huo wakisubiri kujiandikisha muda wanaoutaka wao.

Serikali ilipoanzisha utaratibu huo, ilitoa elimu ya umuhimu wa kuwa na vitambulisho hivyo ambavyo vinamwezesha mtu kupata huduma muhimu ikiwamo kufungua akaunti benki, kupata kadi ya bima ya afya, kupata leseni ya gari, kupata pasipoti ya kusafiria na mambo mengine mengi.

Kwa wanaosafiri kwenda Zanzibar, unapokwenda kukata tiketi ni lazima uonyeshe Kitambulisho cha Taifa na pia unapofika huko, ni lazima uonyeshe kitambulisho hicho ndipo uruhusiwe kuingia.

Kitambulisho hicho pia kinaweza kumsaidia mtu ambaye hajaajiriwa kutumia kumtambulisha anapotaka huduma mbalimbali zinazotolewa na taasisi za serikali au mashirika mengine yanayotoa huduma muhimu kwa wananchi.

Kutokana na umuhimu wa vitambulisho hivyo, kuna baadhi ya watu hivi sasa wanakwama kupata huduma muhimu kwa kutokiwa kuwa na vitambulisho hivyo.

Pia kuna baadhi ya watu ambao wamekwisha jiandikisha kupata vitambulisho hivyo, lakini hawajaenda kuvichukua mpaka wanapotakiwa kuvionyesha wanapotaka huduma ndipo huanza kuhaha kuvifuatilia.

Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), kila mara huwakumbusha wananchi kwenda kuvifuatа vitambulisho vyao kwenye ofisi walizojiandikisha baada ya kukaa muda mrefu bila kuchukuliwa na wenyewe.

Kutokana na umuhimu wa vitambulisho hivyo, wananchi milioni 24 wameshasajiliwa na NIDA kupata vitambulisho hivyo huku Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, akiwahimiza viongozi wa vijiji na mitaa kutoa ushirikiano kwa maofisa wa mamlaka hiyo wakati wa ugawaji wake.

Hivi karibuni ulifanyika uzinduzi wa ugawaji vitambulisho vya NIDA, Musoma mkoani Mara.

Uzinduzi huo ambao ulimjumuisha pia Mkurugenzi Mkuu wa NIDA, Ismail Bumatila, Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda na viongozi wa serikali na maofisa wa mamlaka hiyo wa wilaya sita za mkoa huo, ulihimiza viongozi wa vijiji na mitaa nchini kutoa ushirikiano kwa maofisa wa mamlaka hiyo wakati watakapofika katika maeneo yao kugawa vitambulisho hivyo na kama kuna kasoro ama tatizo watoe taarifa kwa wahusika ili kutatua.

Katika uzinduzi huo wananchi wameelezwa umuhimu mkubwa wa kuwa na vitambulisho hivyo kwa ajili ya kupata huduma za maendeleo na kuwa makini na watu wasio raia kujipatia vitambulisho hivyo kinyume na utaratibu.


Aidha, imeelezwa kuwa serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani imejipanga kufikia Desemba mwaka huu, wananchi waliosajiliwa watakuwa wamepatiwa vitambulisho vyao vya taifa.

Mamlaka hiyo imewahakikishia wananchi kuwa imeongeza kasi ya uzalishaji wa vitambulisho hivyo na vyenye ubora zaidi na inatarajia kuvisambaza na kuvigawa kote nchini na kusisitiza ushirikiano kutoka kwa viongozi wa vitongoji, vijiji na mitaa na wananchi wenyewe ili kazi hiyo iweze kufanikiwa kwa asilimia 100.

Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda aliwaasa maofisa wa NIDA kuvigawa vitambulisho hivyo kwa wananchi ambao ni Watanzania bila vikwazo.

Ni muhimu pia maofisa wa NIDA watakaohusika katika kazi ya ugawaji vitambulisho hivyo kuepuka vitendo vya rushwa wakiwamo viongozi wa vijiji na mitaa kwa kuwa rushwa ni adui wa haki na kutokana na rushwa watu wasio raia wanaweza kujipenyeza kuvipata kinyume na utaratibu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Isiwe kutindua pekee na kujenga pia kuzingatiwe

**PILIKAPILIKA** zimeanza kwa baadhi ya halmashauri kukarabati barabara za vumbi kwa kuzichonga zilizo mbovu na kufukia mashimo ambayo yamejaa maji na kugeuka madimbwi yanayoharibu spiringi za magari na pikipiki.

Ukarabati unazifikia barabara zinazotumiwa na daladala na vituo vya abiria wanaokusanyika kusubiri usafiri sehemu mbalimbali za jiji.

Miongoni mwa halmashauri hizo ni ya Wilaya ya Ilala iliyoko la Dar es Salaam, inayokarabati barabara kuanzia eneo la Kilimanjaro kwenye barabara ya Tabata Chang'ombe ziliko nyumba za Mamlaka ya Mafunzo na Ufundi Stadi (VETA) zikikarabatiwa kwa kuchongwa kwa kufukiwa maeneo yaliyochimbika mashimo madogo na makubwa ili kuondoa madimbwi.

Kumbukumbu zinaonyesha kuwa Barabara ya Tabata Chang'ombe, ilianza kujengwa kwa kiwango cha lami miaka kadhaa iliyopita kuanzia kwenye makutano ya barabara iendayo Segerea eneo la Baracuda.

Ujenzi wake umekuwa ukifanyika kwa awamu hadi Majichumvi -Kisukuru kwenye makutano na ile iendayo Kimara Korogwe na External kupitia jeshini.

Kwenye barabara hiyo mbele kidogo ya kituo cha daladala cha Mwembeni, kulikuwa na dimbwi ambalo lilikuwa likisababisha daladala kusitisha safari na adha kwa watumiaji wa barabara hiyo ya kupita kutokana na kujaa maji.

Makandarasi wanaosimamia ukarabati huo, wamefukia dimbwi hilo na maeneo mengine korofi katika barabara hiyo ili ipitike kwa kipindi chote.

Mbali na ukarabati huo, barabara hiyo itaendelea kujengwa kwa awamu kwa kiwango cha lami hadi Majichumvi Kisukuru na kuunganishwa na inayokwenda External na kukutana na ile ya Mandela.

Ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami ni wa muda mrefu na umekuwa ukifanyika kwa awamu kwa miaka mingi sasa kuanzia kwenye daraja la Vingunguti.

Kuhusu uchongaji wa barabara hiyo, unaoanzia kwenye maeneo ya Kilimanjaro ilipoishia lami, umefanyika na kupita kituo cha daladala Chang'ombe.

Vilevile, umeanzia kwenye makutano ya barabara hiyo kituoni kuelekea barabara zilizopo Mtaa wa Machimbo ambako kuna miinuko na tambarare. Kwenye maeneo hayo, mara nyingi mvua zimekuwa zikisababisha mawasiliano ya barabara kukatika.

Kukarabati barabara kutaleta hamasa kwa wamiliki wa vyombo vya usafiri kuendelea kupeleka magari badala ya kukwepa kutumia barabara hizo kunusuru daladala na bajaj kuharibika na kuingia gharama kubwa za matengenezo.

Barabara zinapopitika mwaka mzima, hurahisisha magari, bajaji na bodaboda kwenda kwenye makazi kutoa huduma za usafiri kwa wagonjwa kuokoa maisha lakini pia abiria, wanafunzi na wafanyabiashara wanaokwenda kwenye majukumu.

Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) mara kwa mara imekuwa ikitoa tahadhari kwa wananchi kuwa huenda kukawa na mvua za kubwa za Elnino wakati wowote kuanzia sasa.

Wengi wanafahamu madhara ya mvua hizo kuwa ni pamoja na kubomoa miundombinu ya barabara, madaraja, makazi na hata viwanda.

Chondechonde barababa hizo zinapokarabatiwa kwa kuchongwa hazijengewi mitaro pembezoni ya kusafirisha maji ya mvua na kusomba udogo, kifusi na hata mchanga, badala ya kubaki mashimo yanageuka kuwa makorongo na si madimbwi tena.

Hutengeneza mabwawa ambayo vyura na mbu huzaliana kwa wingi na kuwa tishio kwa afya za watu.

Furaha ya kuchongewa barabara inakuwa ni ya muda mfupi kwa wakazi wa maeneo hayo ya kupata usafiri na majuto yanakuwa ni ya muda mrefu kwa kukosa huduma hiyo kutokana na kuharibika vibaya zaidi kuliko ilivyokuwa awali.

Pia ni neema kwa baadhi ya vijana kujiajiri kwa kusomba mchanga unaosombwa na maji na kuuza wanaouhitaji kwa ujenzi bila ya kujali kwamba wanachangia kuharibu zaidi barabara na mazingira.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana Ajira na wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako (katikati), akizindua rasmi mpango maalumu kwa ajili ya wastaafu na wastaafu watarajiwa wa Benki ya NMB uitwao NMB Hekima Plan katika hafla maalum iliyofanyika jijini Dodoma. Wa tatu kushoto ni Mkuu wa Idara ya Huduma za Serikali NMB, Vicky Bishubo na wa tatu kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri. Wengine ni Mkuu wa Idara ya Mtandao wa Matawi na Mauzo, Donatus Richard (kushoto), mwakilishi wa wastaafu, Mzee Martine Chiwaligo (kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Kamati yataka ushirikishwaji jamii katika utekelezaji miradi

**Na Christina Haule,** MOROGORO

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira imewaagiza viongozi wa mamlaka za maji nchini kushirikisha jamii kikamilifu na kutoa elimu ya kulinda na kuhifadhi mazingira ili kuleta tija kwenye vyanzo hasa ujenzi wa Bwawa la Kidunda unaoendelea kwa sasa.

Kaimu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Felix Kavejuru, alitoa maagizo hayo juzi wakati kamati hiyo ilipotembelea Bwawa la Kidunda kujionea ujenzi unaoendelea.

Kukamilika kwa bwawa hilo kutaondoa adha ya upatikanaji maji kwa mikoa ya Morogoro, Dar es Salaam na Pwani. Alisema usimamizi wa vyanzo vya maji ni njia ya kufanya vyanzo kuendelea kudumu badala ya kupoteza uwezo au kufa kabisa kutokana na mwingiliano wa shughuli za kibinadamu.

Mratibu wa Mradi wa Maji Bwawa la Kidunda, Christian Gava, alizishauri mamlaka za maji kulinda vyanzo vya maji vinavyopeleka maji na kuleta matokeo sahihi katika mradi huo utakaogharimu zaidi ya Sh. bilioni 329.

Alisema mradi huo utazalisha megawati 20 za umeme. Kati yake, kilovolt 33 zitapelekwa kusaidia vijiji jirani na unaobaki kuingizwa kwenye mkongo wa taifa na hivyo kuchochea maendeleo ya mkoa na nchi kwa ujumla.

Mkurugenzi wa Bodi ya Maji Bonde la Wami Ruvu, Elibariki Mmassy, alisema bwawa hilo pia litatumika kuvuna maji ya mvua ambayo yatasaidia kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa maji katika mikoa tajwa.

Naibu Waziri wa Maji, MarryPriscar Mahundi, alipongeza jitihada za ujenzi wa bwawa ili kukabili ukame kama uliojitokeza mwaka 2020 katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani na kusababisha tatizo kubwa la ukosefu wa maji.

Alisema wanatarajia kusitokee mkwamo wa aina yoyote ili ifikapo mwezi Juni mwaka 2025 sehemu kubwa ya mradi huo ukamilike na kuanza kuingizwa maji kwenye bwawa hilo ili yasipotelee baharini pekee.

Utekelezaji mradi wa Bwawa la Kidunda umeanza baada ya kushindikana kwa zaidi ya miaka 50. Kamati hiyo imeridhishwa na kasi ya ujenzi wake.

# 'Bosi' TANROADS ataja sababu kukumbatia wahandisi wazawa

**Na Beatrice Shayo**

MKURUGENZI Mtendaji wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Mohamed Besta, ametaja faida za kutumia makandarasi na wahandisi wa ndani katika miradi mikubwa inayotekelezwa nchini, ikiwa ni pamoja na kutengeneza ajira nyingi.

Ametaja faida zingine ni kukuza ujuzi, kuboresha ufanisi na kuimarisha ubunifu. Ni katika andiko lake la wiki lililozungumzia kukuza maudhui ya ndani katika sekta ya ujenzi.

Alilitoa kwa vyombo vya habari jijini Dar es Salaam juzi, akisema sekta ya ujenzi ni chachu ya maendeleo kwa kuwa inakuza uchumi na kutengeneza ajira kwa wingi.

"Inafahamika kwamba sehemu kubwa ya ufadhili wa kigeni uliowekezwa katika ujenzi wa miundombinu katika nchi za Kiafrika haunufaishi moja kwa moja makandarasi wa ndani.

"Kuhusisha kampuni za ndani kwenye miradi mikubwa kutakuza uchumi kwa kuzingatia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG)," alisema.

Alibainisha kuwa serikali imetambua hitaji la kuendeleza kampuni za wazawa katika sekta ya ujenzi, akifafanua kuna msukumo mpya kwa makandarasi wazawa na watoa huduma (washauri) kuzingatiwa na kupewa fursa katika miradi ya umma, mchakato wa ujenzi, uendeshaji na utunzaji wa miundombinu unatoa fursa kubwa ya uzalishaji wa ajira nchini.

Besta alisema ushiriki wa kampuni za ndani utasaidia kuendeleza wataalamu wa kizalendo wakiwamo wahandisi, ambao watapata ujuzi wa kuboresha miundombinu inayojengwa.

"Utafiti wa hivi karibuni unakadiria uwekezaji unaohitajika ili kudumisha mali zilizopo Kusini mwa Jangwa la Sahara zinazokadiriwa kuwa asilimia nne ya Pato la Taifa, ni karibu kama uwekezaji unaohitajika kwa miradi mipya ya miundombinu.

"Kuegemea kwa kampuni za kigeni kubuni na kujenga mara nyingi si endelevu kwani utaalamu huo unaweza kuukosa pindi ujenzi utakapokamilika," alifafanua mkurugenzi huyo.

Alishauri kuwa kukuza maudhui ya ndani katika sekta ya ujenzi ni kutumia kampuni za wazawa zilizoajiri wahandisi wa ndani na vifaa vinavyopatikana ndani ya nchi ili kuendeleza ujuzi katika miradi ya ujenzi.

Aligusia mwongozo wa Maudhui ya Kitaifa wa Sekta Mbalimbali uliotolewa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (2019), ambao alisema umeitaja sekta ya ujenzi kama kipaumbele ili kukuza uwezo wa wazawa kushiriki katika miradi mikubwa nchini na katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Alisema pamoja na Bodi ya Makandarasi (CRB) na Wahandisi (ERB) kusajili kampuni mpya kila mwaka, ni kampuni chache za Kitanzania zinazoshiriki miradi mikubwa ya ujenzi wa barabara kuu, madaraja, miundombinu mirefu au vifaa vya kiufundi kama vile viwanda, madini na miradi ya reli.

"Ni dhahiri kwamba sera za maudhui ya ndani, mikakati na rasilimali ni nyenzo muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi, kuongeza ajira na fursa kwa kampuni za ndani ya ujenzi kuhamisha teknolojia na utaalamu wa kiufundi ambao ni muhimu kwa taifa," alisema.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MRADI WA UENDELEZAJI WA BONDE LA MSIMBAZI**
**(IDA CREDIT NO. 7215-TA)**

# TANGAZO KWA UMMA

## ZOEZI LA ULIPAJI FIDIA KWA WATU WANAOATHIRIKA NA MRADI

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) inatekeleza mradi wa uendelezaji wa Bonde la Msimbazi kwa lengo la kukabiliana na mafuriko na kuboresha matumizi ya ardhi katika eneo la chini la bonde. Ili kufanikisha utekelezaji wa mradi, Serikali inatarajia kuwahamisha watu wote wanaoathirika na mradi kwa kuwalipa fidia ya mali zao zinazoathirika.

Mthamini Mkuu wa Serikali ameshaidhinisha jedwali la fidia lililozingatia maoni yake na wadau wengine, na sasa zoezi la ulipaji fidia linatarajiwa kuanza mapema iwezekanavyo. Ikumbukwe kuwa jedwali hili la fidia linawahusu waathirika wa mradi walioafiki fidia zao wakati wa zoezi la kuhakiki fidia lililofanyika mwezi Machi 2023.

Kampuni ya kusimamia ulipaji wa fidia (PROPERTY MATRIX LIMITED), inayofanya kazi kwa niaba ya OR-TAMISEMI, inatarajia kufanya zoezi la kusainisha mikataba ya malipo ya fidia pamoja na kuhakiki taarifa za benki kabla ya kufanya malipo. Kampuni hii itafanya zoezi hili katika kila Kata kwa ratiba ifuatayo:

| Eneo la Usainishwaji | Kata | Mitaa Inayohusika | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Ukumbi wa DRIMP (Ilala Kota) | Mchikichini | Msimbazi Bondeni | 18 hadi 20/10/2023 |
| | | Misheni Kota | 21 na 22/10/2023 |
| | | Ilala Kota | |
| | Kariakoo | Kariakoo Kasikazini | |
| | Upanga Magharibi | Charambe | 31/10/2023 hadi 02/11/2023 |
| | Jangwani | Mtambani A | |
| | | Mtambani B | |
| | | Jangwani | |
| Ofisi ya Kata - Magomeni | Magomeni | Suna | 23 hadi 25/10/2023 |
| Ofisi ya Kata - Mzimuni | Mzimuni | Idrisa | 26/10/2023 |
| | | Mtambani | |
| | | Mwinyi Mkuu | |
| Shule ya Msingi Mapinduzi - Kigogo | Kigogo | Kigogo Mbuyuni | 27 na 28/10/2023 |
| | Hananasif | Mkunguni A | 29 na 30/10/2023 |
| | | Mkunguni B | |
| | | Hananasif | |
| Ukumbi wa DRIMP (Ilala Kota) | | Kawawa | 3 hadi 5/11/2-23 |

Wahusika wanaombwa kufika katika maeneo ya usainishwaji wakiwa na vitambulisho (NIDA/Uchaguzi) na nyaraka zote zinazowathibitisha iwapo wanapokea malipo kwa niaba.

**KATIBU MKUU**
**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MRADI WA UENDELEZAJI WA BONDE LA MSIMBAZI**
**(IDA CREDIT NO. 7215-TA)**

# TANGAZO KWA UMMA

## ZOEZI LA UHAKIKI WA MALI ZILIZOATHIRIKA NA MRADI KWA WATU AMBAO HAWAKUAFIKI VIWANGO VYA FIDIA NA WALIOSAJILI MALALAMIKO

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) inatekeleza mradi wa uendelezaji wa Bonde la Msimbazi kwa lengo la kukabiliana na mafuriko na kuboresha matumizi ya ardhi katika eneo la chini la bonde. Ili kufanikisha utekelezaji wa mradi, Serikali inatarajia kuwahamisha watu wote wanaoathirika na mradi kwa kuwalipa fidia ya mali zao zinazoathirika.

Kufuatia zoezi la uhakiki wa fidia lililofanyika mwezi Machi 2023, baadhi ya waathirika wa mradi hawakuafiki viwango vya fidia walivyo onyeshwa, na baadhi walisaini kuridhia viwango vya fidia na kisha kuandika barua za malalamiko. Katika kushughulikia malalamiko yao, OR-TAMISEMI inatarajia kufanya zoezi la kuhakiki upya mali za waathirika hao kwa kuzingatia aina ya malalamiko yao. Kutakuwa na timu mbili za wathamini kwa wilaya za Kinondoni na Ilala ambazo zitapita kwenye makazi ya waathirika husika kwa ratiba ifuatayo:

| Tarehe | Mtaa Itakayotembelewa | |
|---|---|---|
| | Timu ya Ilala | Timu ya Kinondoni |
| 19 na 20/10/2023 | Msimbazi Bondeni | Kigogo Mbuyuni |
| 23 na 24/10/2023 | Charambe | Hananasif |
| | Ilala Kota | Mkunguni A |
| | Mtambani A | Mkunguni B |
| | Mtambani B | Idrisa |
| | Kariakoo Kaskazini | Suna |
| | | Mwinyimkuu |

Wahusika wanaombwa kutoa ushirikiano kwa kuwepo katika ofisi za Serikali za Mitaa yao kuanzia saa 2:00 asubuhi.

**KATIBU MKUU**
**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**



# MoCU yawapa 'rungu' wenyeviti mitaa, vijiji kuwakamata wanafunzi wazururaji

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

CHUO Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), kimewapa 'turufu' wenyeviti wa serikali za mitaa na vijiji wanaokizunguka chuo hicho, kuwachukulia hatua wanafunzi wanaokamatwa na sungusungu usiku wa manane, wakisingizia wametoka chuoni kusoma.

Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Wanafunzi wa MoCU, Dk. Elisifa Nnko, akizungumza jana na wadau wanaotoa huduma mbalimbali kwa wanafunzi nje ya chuo hicho, alisema hata kwa wanafunzi wanaolala ndani ya chuo hicho, ikifika saa 6:00 usiku, hakuna mwanafunzi anayeruhusiwa kuonekana nje.

"Kila mwanafunzi wetu ana kitambulisho kinachotolewa na taasisi. Kwa hiyo, kusiwe na kisingizio kwamba umekutana na mwanafunzi saa saba usiku, saa nane ya usiku, akakuambia mimi ni mwanafunzi wa MoCU, hana kitambulisho, mkamate.

"Wanafunzi wengine unakutana nao huko saa saba usiku, saa tisa usiku wanakamatwa na sungusungu wanasema tulikuwa chuoni tunasoma. Sio kweli, sisi tuna muda maalum wa wanafunzi kukaa nje ya mabweni.

...Walinzi wetu ikifika saa 6:00 usiku wanajua na serikali ya wanafunzi wanajua kwamba, ikifika muda huo hakuna mwanafunzi anayetakiwa kuonekana nje ya mabweni."

Kati ya wanafunzi 9,000 waliopo katika chuo hicho, wanaopata nafasi za malazi ndani ya chuo ni 1,200. Zaidi ya 7,000 wanafunzi wanaishi nje ya chuo wakiwa wamepanga hosteli.

Kwa mujibu wa Dk. Nnko, MoCU inayo sheria ambayo huhamasisha wanafunzi wao wasitembee mmoja mmoja usiku, na huo huwa ni wimbo wao kila wakati.

Aidha, amewashauri wamiliki wa hosteli zinazotoa huduma ya malazi kwa wanafunzi wa chuo hicho, kuweka sheria kali za kuwabana wanafunzi waliopanga kwao kutoingia kwenye hosteli zao, baada ya saa 4:00 usiku.

Katika kikao hicho kilichoongozwa na Diwani wa Kata ya Rau, Manispaa ya Moshi, William Kiwia, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Kariwa Chini, Thomas Materu, alieleza namna wanavyopata tabu ya kuwatambua wanafunzi wanaokamatwa na sungusungu usiku wa manane, wakidai ni wanafunzi wa MoCU, lakini ukichunguza wengine sio wanafunzi.




Waziri wa Afya ambaye ni Mbunge wa Tanga Mjini, Ummy Mwalimu (wa pili kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Coca-Cola, Unguu Salum (aliyevaa koti), wakikabidhi vitendea kazi kwa wanufaika 311 wa programu ya Mwanamke Shujaa ya Coca-Cola katika hafla iliyofanyika mjini Tanga juzi. Programu hiyo ina lengo la kuwawezesha wanawake kiuchumi, wengi wakijishughulisha na biashara ya mamalishe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tabia vijana Kilimanjaro kupenda pombe kali yamsikitisha RC

**Na Mary Mosha** MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, ameeleza masikitiko yake ya namna anavyochukizwa na idadi kubwa ya vijana wa mkoa huo kuendekeza unywaji wa pombe kali.

Akizungumza jana katika eneo la Manyema, Manispaa ya Moshi, alikokwenda kufungua wiki ya utoaji wa huduma za afya bure kwa wananchi, Babu alisema afya za vijana wengi haziridhishi kutokana na kuathiriwa na unywaji wa pombe.

Kutokana na ongezeko la athari za wagonjwa wa figo, Babu, amekemea unywaji wa pombe kupita kiasi, akiwataka vijana kuacha matumizi makubwa ya pombe kali, kwa kuwa husababisha figo kushindwa kufanya kazi, pamoja na kuwapo ongezeko la shinikizo la damu na sukari.

"Badilisheni mfumo wa ulaji, tujitahidi katika kufanya mazoezi angalau kwa dakika 30 kila siku, na unapojisikia hali ya tofauti wai katika hospitali iliyopo karibu nawe," alisema Babu. Huduma hiyo imepangwa kutolewa kwa siku tatu na Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro ya Mawenzi.

Awali, Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. EdnaJoy Munisi, alimweleza Babu kuwa katika kila wagonjwa 10 wanaonwa na madaktari wa hospitali hiyo, saba kati yao hugundulika kuwa na magonjwa yasiyoambukizwa.

Magonjwa hayo ni kisukari, shinikizo la damu na uzito uliopitiliza, ambayo huchangiwa na mfumo mbaya wa ulaji wa vyakula, kutofanya mazoezi na matumizi ya pombe kali kupitiliza.

Dk. Munisi, alisema mkakati wa hospitali hiyo ni kuwafikia wagonjwa 2,500 wa Mkoa wa Kilimanjaro.

"Ukiwa na ugonjwa kama shinikizo la damu, sukari na uzito kupitiliza, unaweza kuchangia matatizo mengi yakiwemo ya ngozi, upofu, kushindwa kufanyakazi kwa figo, matatizo ya macho pamoja na meno," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Munisi, katika Mkoa wa Kilimanjaro, kumekuwapo na ongezeko la magonjwa ya saratani.

Mmoja wa watu waliojitokeza kufanyiwa uchunguzi wa kitabibu, Elinathan Kweka, alisema matibabu hayo yanapaswa kufanywa kila mwisho wa mwezi, huku akishauri serikali kuanzisha huduma mkoba za afya kwa kila wilaya.

## Watoto 10,000 wafanyiwa ukatili kipindi cha mwaka mmoja

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amesema watoto zaidi ya 10,000 nchini wamekumbana na madhila ya ukatili wa kingono katika kipindi cha mwaka mmoja.

Amesema watoto hao wa kike waliobakwa ni kati ya watoto 12,000 walifonyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia katika maeneo mbalimbali nchini.

Alitoa takwimu hizo juzi mkoani Arusha wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kitaifa ya Mwanamke anayeishi kijijini.

Maadhimisho hayo yalibeba kauli mbiu isemayo, 'Wezesha wanawake waishio kijijini kwa uhakika wa chakula, lishe na uendelevu wa familia'.

Aidha, ameagiza maofisa maendeleo ya jamii nchini kuongeza kasi zaidi ya kuyafikia makundi ya wanawake wajasiriamali wanaoishi vijijini, ili kuwaunganisha na fursa za mifuko na programu za kuwakwamua wanawake kiuchumi.


"Wanawake wengi wanaonewa na kunyanyaswa kwa kufanyiwa vitendo vya aina mbalimbali za ukatili. Ifike wakati jamii itafakari kwa kupata mawazo mbadala wa watoto pamoja na wanawake ili waishi kwa amani, kila familia ijenge utaratibu wa kurejesha maadili mema kuanzia katika malezi na makuzi, kwa sababu idadi ya wanawake na watoto wanaofanyiwa vitendo vya ukatili ni kumbwa mno," alisema Dk. Gwajima.

Kuhusu kuwaunganisha wanawake wa vijijini na fursa za kiuchumi, Dk. Gwajima, alisema Rais Samia Suluhu Hasaan, katika kutambua umuhimu wa wanawake, ameanzisha mifuko saba ya kuwakwamua wanawake kiuchumi, katika taasisi mbalimbali za fedha.

Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Amon Mpanju, alisema maadhimisho hayo yanakwenda sambamba na wanawake wa vijiji na kata zote nchini, kupata fursa ya kupewa elimu ya uzalishaji wa chakula Ili kuboresha lishe itakayokuwa na familia bora.

Awali, Askofu wa Kanisa la Kilutheri la Afrika Mashariki (KKAM), Dk. Filemon Mollel, aliiomba serikali kuendelea kulinda kizazi cha vijana, kutokana na mmomonyoko mkubwa wa maadili hasa watoto wa kiume, ambao wanafanyiwa vitendo vya kikatili kwa asilimia kubwa kuliko wakike.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Olevolos, Emmanuel Lesioni, aliiomba serikali kuwajengea kituo cha afya kutokana na wanawake wa kijiji hicho, kutembelea umbali wa kilomita 30 kwenda Hospitali ya Wilaya ya Oltrumet, kwa ajili ya kujifungua.





# RC aagiza matokeo ya sensa yatumike kuleta maendeleo

**Na Remmy Moka,** SAUT

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla, amewaagiza watumishi mkoani hapa kuhakikisha wanatumia matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 kuleta tija ya maendeleo katika mkoa.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na watumishi wa umma na binafsi, wadau wa maendeleo na vikosi vya ulinzi na usalama pamoja na viongozi wa dini wa Mkoa wa Mwanza baada ya kupata mafunzo ya usambazaji na matumizi ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022.

Aliwataka kuhakikisha wanatumia matokeo hayo kujua maeneo yenye uhitaji wa huduma za kijamii kama vile umeme, maji na barabara na pia maeneo yasiyo na huduma za kijamii ili ziwafikie haraka.

"Mkitumia matokeo haya kwa ufanisi mkubwa itasaidia kuinua uchumi wa mkoa wetu kwa kutatua kero mbalimbali zilizoibuliwa na matokeo haya ndani ya jamii na kuleta majawabu ili kukuza uchumi na kuchochea maendeleo kwa ujumla," alisema Makalla.

Kaimu Meneja wa Idara ya Takwimu, Benedict Mugambi, alieleza kuwa lengo la kutoa elimu kwa makundi hayo ni kuwasaidia juu ya namna ya kutumia takwimu ya sensa katika mipango mbali mbali ya maendeleo.

Baadhi ya viongozi wa dini waliohudhuria mafunzo hayo waliishukuru serikali kwa kufanya sensa kwa ubora ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya namna ya kutumia matokeo ya takwimu kwa ajili ya maendeleo.

Kwa mujibu wa matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, Tanzania ina watu milioni 61.7, huku Mkoa wa Njombe ukishika nafasi ya mwisho kuwa na idadi ndogo ya wananchi wapatao 900,000 na kwa upande wa Zanzibar Mkoa wa Kusini Unguja una idadi ndogo ya watu 200,000.




Mkuu wa Wilaya ya Kwimba, Ng'wilabuza Ludigija (wa tatu kulia), akizindua tawi la Benki ya CRDB lililoko Ngudu mwishoni mwa wiki. Tawi hilo linakuwa la 18 mkoani Mwanza na la 261 nchi nzima. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Silinde atuma salamu kwa wahujumu mbolea ya ruzuku

**Na Halima Ikunji,** TABORA

NAIBU Waziri wa Kilimo, David Silinde, ameitaka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kuchukua hatua kali na za kisheria kwa yeyote atakayethibitika kufanya vitendo vinavyohujumu mpango wa utoaji wa mbolea ya ruzuku kwa wakulima.

Alitoa agizo hilo juzi katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mbolea Duniani yaliyofanyika kwenye viwanja vya Chipukizi mkoani Tabora na kueleza kuwa utolewaji wa mbolea ya ruzuku ni mpango wa serikali kumsaidia mkulima.

Alisema lengo la mpango huo ni kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi zinazojitosheleza kwa chakula duniani, ambapo ulianza tangu nchi kupata uhuru wake mwaka 1961.

Silinde alieleza kuwa ili kuhakikisha wakulima wanaongeza uzalishaji wa mazao, serikali imeendelea kuweka mipango mbalimbali ya kuweza kuwasaidia kundi hilo kufikia malengo binafsi.

Aidha, alibainisha kuwa serikali imeweka mfumo wa kielektroniki ambao unaratibu usajili wa wakulima nchini ili kupunguza mianya ya udanganyifu na kuwaweka wazi katika utekelezaji wa mpango wa utoaji huduma ya mbolea ya ruzuku.

Pia alitoa wito kwa wakulima nchini ambao hawajajiandikisha kwenye mfumo wafanye hivyo na wale waliojiandikisha msimu wa mwaka 2022/23 wakahuishe taarifa zao kwa ajili ya maandalizi ya msimu wa mwaka 2023/24 ambao tayari umeanza.

Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Joel Laurent alisema katika kutekeleza majukumu yake mamlaka imekuwa na mafanikio mbalimbali ambapo imeyafikia ikiwa ni pamoja na kuimarisha ukaguzi wa mbolea kwa kuanzisha na kuimarisha ofisi tano.

Laurent alisema wameendelea kuimarisha mifumo ya udhibiti wa mbolea ili kuhakikisha wakulima wanapata mbolea bora wakati wote ili kuwasaidia kuboresha shughuli zao za kilimo.

Alisema lengo waliojiwekea ni kufanya ukaguzi kwa wafanyabiashara 2,950 katika kanda zote tano na tayari wamefanikiwa kuongeza aina ya mbolea zilizosajiliwa kwa mwaka 2018/19.

# Mavunde atangaza neema kwa vijana wachimbaji madini

**Shaban Njia na Mohab Dominick**

WAZIRI wa Madini, Antony Mavunde, amesema serikali ipo katika mpango maalumu na taasisi za kifedha nchini utakaosaidia kuwafungulia milango ya kuwakopesha vijana, wafanyabiashara katika sekta ya madini.

Mavunde alitoa kauli hiyo hivi karibuni akiwa ziarani wilayani Kahama na kueleza kuwa shughuli za uchimbaji madini wa kuhamahama unasababisha kukosa imani ya kukopesheka na taasisi za kifedha.

Aidha, alieleza kuwa sababu hiyo imemfanya akutane na taasisi hizo na kujadili ni namna gani watawafikia na kuyakopesha makundi hayo kukuza sekta ya madini na vijana kuacha kutegemea ajira serikalini.

Mavunde alisema miaka ya nyuma aliwahi kuwa kiongozi wa FEMATA na anafahamu namna gani wachimbaji wadogo na wafanyabiashara wa madini hususani vijana wanavyopata changamoto katika shughuli zao.

Hivyo aliahidi kufanya mkutano hivi karibuni na kusikiliza kero za wachimbaji na wafanyabiashara hao. Aidha, Mavunde alifurahishwa na idadi kubwa ya vijana wanaochangamkia fursa na uchumi wa madini kwa kuchimba, kununua na kuuza madini ili kuondokana na dhana ya kuendelea kutegemea ajira kutoka serikalini.

Alisema kuwa hakutegemea kukutana na wafanyabiashara wa madini vijana katika masoko makuu ya dhahabu na kusema hali hiyo inaonyesha kuwa wametambua fursa za sasa kujiajili kupitia sekta hiyo, hivyo upo umuhimu wa kutimiza ndoto zao.

Mwenyekiti wa Soko Kuu la Madini Kahama, Emmanuel Kidenya, alikili kuwapo kwa changamoto ya upatikanaji wa mikopo hususani kwa vijana na wamekuwa wakijichanga kwa vikundi na wakati mwingine kuweka lehani nyumba zao kwa lengo la kupata mitaji.

Alisema kwa sasa wanaendelea na zoezi la kuhakikisha hakuna kijana anayejihusisha na utoroshaji wa madini na kwenda kuuza kinyemela wakiwasisitiza katika vikao ambavyo amekuwa akivifanya na wafanyabiashara hao na wale wanaobainika wanaripotiwa ofisi za madini kwa hatua zaidi.

Mmoja wa wafanyabiashara wa madini ambaye ni kijana, Yasini Salumu alisema hawana mitaji mikubwa ya kufanya biashara hizo na badala yake wanalazimika kujiunga kama kikundi ili kufanikisha kupata mitaji kwa kila mmoja kuuza au kuweka lehani kile alichonacho na faida wanayoipata mwisho wa mauzo wanagawana.



Ukurasa 12

Mkutano kutokomeza ukeketaji uamshe mabadiliko mikoa vinara



Ukurasa 13

Wakati mamilioni hawavutiwi kusoma, mbinu zatajwa kuwarejesha kundini

Nipashe
TESA
Jumanne Oktoba 17, 2023
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

**Zijue mbinu za kuacha kuhaha kusaka usingizi mwororo usiku**

ELIMU
NA SABATO
KASIKA

# Wanafunzi wanavyochefukwa na vigodoro kuaibisha, kudhalilisha utu

• Vyatajwa chanzo kuwanyanyasa watoto wa kike, kiume kingono

VIGODORO ni ngoma za ukanda wa pwani, zinaweza kufananishwa na ukengeufu kutokana na baadhi ya wanawake kucheza utupu wakionyesha maungo ya siri tena mbele za watu wa rika tofauti kuanzia watoto hadi wazee.

Ni ngoma inayochezwa katika mazingira 'machafu' wengine wakicheza utupu, hukatika kupindukia, huongea matusi muda wote na pia wapo wanaofanya ngono hadharani.

"Mabinti na watoto wanaokwenda katika ngoma hizo, wengine hubakwa, kulawitiwa, kuingiliwa kinyume cha maumbile, kuambukizwa maradhi ya ngono na kupata mimba za utotoni. Ingependeza ikipigwa marufuku," anasema Hawa Rashid, mwanafunzi wa kidato cha tatu, wa Sekondari ya Mzimuni iliyopo Dar es Salaam.





Mwanafunzi Hawa Rashid akichangia hoja. **PICHA: SABATO KASIKA**

Anaongeza: "Mabinti wanaotoka katika familia zenye malezi duni hawazuiliwi kushiriki vigodoro usiku hukutwa na mabalaa mengi," anaongeza.

Ni wakati wa kuchangia hoja kwenye kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kike Duniani, yanayoandaliwa na asasi ya Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), yanayofanyika Dar es Salaam.

Maadhimisho yanawaleta pamoja washiriki kutoka polisi, TAKUKURU, asasi za kiraia, serikali na wanafunzi kutoka sekondari na msingi.

Anaungwa mkono na mwanafunzi mwenzake Sekela Mwakyusa, anayesoma Chuo cha Don Bosco, anayesema kuwa ngoma za vigodoro, wanawake wanacheza nusu uchi na kusababisha wanaume wanaohudhuria kuwaka tamaa kitendo kinachosababisha wabake watoto wa kike ili kukidhi tamaa zao.

Anasema ipo haja kwa wazazi na walezi kusimamia malezi bora kwa watoto wao, ili waepuke kwenda katika ngoma za vigodoro.

"Lakini ni vyema kila shule kuwa na klabu ya kupinga ukatili kwani matendo hayo hutokea, nyumbani, mitaani na shuleni, kwa hiyo klabu hizo zikiwapo wanafunzi wanaweza kujifunza mbinu za kuyakabili," anasema Sekela.

Anasema mtoto wa kike anawindwa kila kona na kwamba jitihada za kumlinda zinahitajika kuanzia kwa wazazi, walezi, walimu na jamii kwa ujumla, ili aweze kutimiza malengo yake ya maisha aliyojiwekea.

### SAUTI YA POLISI

Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Wilaya ya Kinondoni, Makala Khida, anawakumbusha wanajamii kuwa iwapo mwanamke atabakwa anatakiwa asinawe wala kuoga kuhifadhi ushahidi.

"Ukifanyiwa vitendo hivyo, usioge wala kubadilisha nguo, acha hali ibaki kama ilivyo ila fika polisi upewe fomu namba tatu PF-3 kisha nenda hospitali kupata vipimo baada ya hapo hatua nyingine zifuate," anasema Khida.

Anafafanua kuwa katika mazingira hayo, ushahidi wa tukio unapatikana na kwamba baadhi ya watu huupoteza kwa kutojua wakidhani mwathirika akioga na kubadilisha nguo hautapotea.

"Hapa kuna utaalamu wa kisayansi unatumika, sisi polisi tunahusika na madaktari nao wanahusika katika kumbaini mtuhumiwa wa vitendo vya ubakaji, hivyo wito wangu linapotokea tukio hilo, aliyetendewa asioge wala kubadilisha mavazi," anasema.

Mwakilishi wa Mkuu wa TAKUKURU Wilaya ya Kinondoni, Agness Msumari anasema, vita dhidi ya ukatili wa kijinsia kwa mtoto itakwisha jamii itakapotambua umuhimu wa vita hiyo.

"Hivyo kinachotakiwa ni utoaji wa elimu kwa jamii kuhusu madhara ya vitendo hivyo ikiwamo rushwa ya ngono, ofisi zetu ziko wazi kwa mwenye taarifa za kila aina za rushwa," anasema Agness.

Aidha, anawataka wazazi na walezi kuzingatia maelezi mema ili kuwaepusha watoto wao na vitendo hivyo vinavyohatarisha maisha, hasa kwenda kwenye ngoma za vigodoro usiku.

### WAZAZI NI KIKWAZO

Mratibu wa Elimu Kata ya Makumbusho, Sylvester Milobo, anasema baadhi ya wazazi na walezi ni kikwazo katika vita ya kukomesha ukatili wa watoto na kwamba watoto wanafanyiana wenyewe kwa wenyewe hata shuleni au kufanyiwa na watu wengine, lakini wazazi wao wakiitwa kuelezwa hawataki wanadai wanasingiziwa," anasema Milobo.

Anasema wazazi na walezi hao wanakwamisha mikakati ya kutokomeza ukatili na kwamba wengine wapo tayari kupokea kitu kidogo kutoka kwa watuhumiwa ili mambo yaishe kimya kimya.

Riziki Mwambusi ni Ofisa Maendeleo ya Jamii Kata ya Makumbusho ambaye anakiri kwamba vitendo vya ukatili kwa watoto wa kike na kiumbe bado vinatokea katika za kata.

INAENDELEA UK.14

ELIMU

NA REUBENI LUMBAGALA

# Mkutano kutokomeza ukeketaji uamshe mabadiliko mikoa vinara



Zana asilia zinazotumiwa kukeketa wanawake. **PICHA: MTANDAO**

UKATILI dhidi ya kiumbe chochote iwe ni wanadamu, wanyama. Mdudu au ndege haukubaliki kwa watetezi wa haki.

Kila kilichoumbwa kina haki ya kufurahia maisha na kushangilia uumbaji na binadamu kama kiumbehai mwenye akili, utashi, uwezo mkubwa wa kufikiri na kutafakari aliyepewa mamlaka ya kutawala vingine anapaswa kuwa mfano wa kulinda na kuheshima haki za wote.

Dunia ya leo inakabiliwa na changamoto kubwa ya ukatili dhidi ya watu na viumbe na mazingira.

Ukatili huo umekuwa ukifanywa na binadamu dhidi ya wanadamu wenzake. Kuwakatili wengine kunakofanywa na binadamu leo kunahusisha ubakaji, ulawiti, kuingiliwa kinyume cha maumbile, ukeketaji, ndoa za utotoni, mauaji na vipigo kwa watoto na wenza wa ndoa.

Mengine ni kupora wajane mali na watoto, kuwafukuza kwenye ardhi zao, kuwatesa yatima na watoto wahitaji, kutesa wanaoishi na ulemavu kama kuwafungia watoto ndani na kutesa wazee.

Kutokana na ongezeko la vitendo vya kikatili duniani na hasa katika nchi zinazoendelea, juhudi madhubuti zimechukuliwa kitaifa na kimataifa kwa kuhakikisha kunakuwapo na mijadala mbalimbali ili kuja na maazimio ya pamoja na namna bora ya kumaliza vitendo vya kikatili ambavyo ni adui wa kufanikisha mipango mingi ya maendeleo.

> Jamii katika mikoa hiyo vinara wa ukeketaji wanapaswa kubadilika kwani mila hii potofu imepitwa na wakati, waachane nayo kulinda afya na utu wa mwanamke.

Hivi karibuni Tanzania ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa Pili wa Kimataifa wa Kutokomeza Ukeketaji wa wanachama wa Umoja wa Afrika (AU).

Ukifanyika jijini Dar es Salaam, mkutano huo unaoanza Oktoba 9 hadi 11 mwaka huu, unakusanya zaidi ya washiriki 900 wakitokea maeneo mbalimbali duniani kati yao 200 ni washiriki wa ndani na 700 ni kutoka mataifa mengine.

Ajenda kubwa ikiwa ni kuunganisha nguvu ya pamoja dhidi ya vitendo vya ukeketaji ambavyo ni sehemu ya ukatili dhidi ya wasichana na wanawake. Mkutano huu unachagizwa na kaulimbiu isemayo, "mabadiliko katika kizazi kimoja kwenda kingine ni muhimu katika kutokomeza vitendo vya ukeketaji."

Aidha, katika mkutano huo, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, anasema takwimu zinaonyesha kuwa wanawake na watoto wa kike milioni 200 duniani wamekeketwa huku milioni 20 wakifanyiwa dhuluma hiyo na wataalamu wa afya na watoto wa kike milioni 60 wakiwa wapo katika hatari ya kukeketwa.

Inamaanisha kuwa takwimu hizo hazilete furaha ni za kutisha zikihusisha vitendo vya ukeketaji. Pia ni jambo la kushangaza kuona wataalamu wa afya wanashiriki vitendo vya ukeketaji ambapo kwa watoa huduma hao walipaswa kujiepusha na vitendo hivyo kutokana na kuwa na uelewa mkubwa wa athari za ukeketaji.

Vilevile, katika mkutano huo, Waziri Gwajima anasema, ukeketaji unaondoa utu wa mtoto wa kike na wanawake, kila msichana anaweza kukua bila kufanyiwa ukeketaji, hatuwezi kufikia dira ya maendeleo ya Tanzania 2030 ikiwa mamilioni ya wasichana wataendelea kufanyiwa ukatili wa kijinsia. Lazima tuseme inatosha ili kulinda wanawake milioni 68 walio katika hatari ya kukeketwa."

Pia, kwa mujibu wa takwimu za Umoja wa Mataifa za mwaka 2022, wasichana na wanawake wenye umri wa miaka 15 hadi 49 wamekeketwa na asilimia 35 wamekeketwa wakiwa hawajafikia umri wa mwaka mmoja huku katika wanawake 10 mmoja akiwa amekeketwa.

Takwimu hizi ni wito kwa kila mwanajamii kushiriki kikamilifu katika mapambano ya kutokomeza ukeketaji na ukatili dhidi ya watoto wa kike, wasichana na wanawake ili kuwajengea mustakabali mwema wa maisha yao.

Pamoja na uwepo wa vitendo vya ukeketaji vinavyochangiwa na mila potofu lakini ni jambo la faraja kuona Tanzania imepiga hatua kubwa katika mapambano dhidi ya matendo hayo.

Kwa mujibu wa Kamishna wa Afya, Haki za Binadamu na Maendeleo ya Jamii (HHS) wa Umoja wa Afrika, Balozi Minate Samate, akizungumza kwenye mkutano huo, anasema Tanzania imepunguza ukeketaji kwa asilimia 75 huku ikiwa miongoni mwa nchi zenye viwango vya chini vya ukeketaji ikiwa na asilimia 15.

Pamoja na mafanikio haya, taifa halipaswi kubweteka kwani ni wakati wa kutokomeza ukeketaji na kufikisha asilimia ziro. Kuendeleza ukeketaji ni kurudisha nyuma juhudi kubwa zinazofanywa na serikali pamoja na wadau wengine wa maendeleo za kumkomboa mwanamke kijamii na kiuchumi. Takwimu za Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF), zinaonyesha ukeketaji katika mikoa ya Manyara ni asilimia 58, Dodoma 47, Arusha 42, Mara ni asilimia 32 wakati Singida ni 31 na Tanga asilimia 14.

Jamii katika mikoa hiyo vinara wa ukeketaji wanapaswa kubadilika kwani mila hii potofu imepitwa na wakati, waachane nayo kulinda afya na utu wa mwanamke.

Wanaume kwa upande wao wanayo nafasi kubwa ya kufanikisha mapambano ya ukeketaji kwani kama watakataa kuoa wanawake waliokeketwa, ni dhahiri wazazi na walezi wakatakaa mabinti na wategemezi wao wa kike kufanyiwa matendo hayo.

Kuendeleza utamaduni wa kukeketa watoto wa kike ili waolewe, ni kuchochea kuendeleza utamaduni huo kurudisha nyuma maendeleo.

Ni vyema jamii kubadilika, kukataa ukeketaji na ukatili wa kijinsia iwe mijini na vijijini kwa kuwa ni udhalilishaji na ukandamizi usio na tija.

***Mwandishi ni Mwalimu wa Mlali Sekondari mkoani Dodoma.***

***Maoni: 0620 800 462.***

ELIMU
NA JULIETH MKIRERI

# Wakati mamilioni hawavutiwi kusoma, mbinu zatajwa kuwarejesha kundini

JUHUDI za kukumbusha watu umuhimu wa kusoma kama kigezo cha msingi ili kuongeza ufahamu, ujuzi, heshima na kudumisha utu na haki za binadamu ni suala endelevu, linathibitishwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO).

Ndiyo maana kila mwaka Septemba 8, ni Siku ya Usomaji Duniani, jambo linaloelezwa kuwa na tija, na sasa wakati dunia ikiadhimisha siku ya kujua kusoma na kuandika UNESCO inasema kumekuwa na hatua kubwa katika kufikia azma hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa ya shirika hilo ya Septemba 8 mwaka huu, licha ya kazi kubwa kufanyika, kujua kusoma na kuandika kunahitajika ili kuwafikia watu milioni 763 duniani ambao ni mbumbumbu.

Pamoja na hali hiyo wanaofahamu wameongezeka ingawa juhudi zaidi zinahitajika, linasema shirika hilo.

Mwakilishi wa Kamishna wa Elimu, kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Hawa Selemani, anasema siku ya usomaji huileta jamii pamoja katika kujadili vikwazo vinavyochangia kutokujua kusoma na kuandika katika maeneo yao.

"Siku hii huangazia ukweli kwamba bado kuna mamilioni ya wasiojua kusoma na kuandika lakini hata leo na wapo ambao hawana tabia ya kujisomea. Aidha, hulenga kujenga uelewa wa pamoja kwenye jamii kuhusu umuhimu wa kusoma na kuandika ambao ndiyo msingi wa tabia ya usomaji na ujifunzaji," anaeleza Hawa.

Akiwa katika kongamano la usomaji linaloandaliwa na Shirika la Kimataifa la Room to Read, anasema ni muhimu kuboresha mbinu za kufundisha na kujifunza KKK katika kujenga stadi za kusoma kwa wanafunzi wa shule za msingi.

Hata hivyo, anasema kujua kusoma na kuandika pekee hakutoshelezi kumfanya mwanafunzi kuwa mahiri na mwenye kupenda kujisomea na hivyo wanatakiwa kupata fursa ya kusoma vitabu kwenye maktaba kukuza stadi na kujenga tabia ya usomaji."

Sambamba na hayo anaeleza kwamba mwanafunzi anapokuwa msomaji wa kujitegemea anakuwa na uwezo mkubwa wa kusoma kwa ufasaha kwa kasi stahiki na kuonyesha hisia.

"Kwa upande mwingine kutojua KKK hupunguza ari ya kusoma na kujifunza kwa mtoto, humfanya kuwa na mahudhurio hafifu na hata kuacha chule hivyo kukatisha ndoto zake," anasema.



Wanafunzi wakiendelea kufurahia kusoma vitabu mbalimbali vya hadithi mkoani Pwani. **PICHA: JULIETH MKIRERI**

Kadhalika, anasema serikali inaendelea na juhudi za kuboresha elimu nchini na kuondoa tatizo la kutojua kusoma na kuandika jitihada ambazo zinakwenda sambamba na kufundishana kujifunza KKK.

Vilevile anasema ili mwanafunzi afanikiwe akiwa shuleni na baada ya shule inabidi amudu stadi za kujifunza akieleza kuwa karne ya 21 inahusu fikra tunduizi, ubunifu, mawasiliano na ushirikiano kupitia kusoma vitabu vya mambo mbalimbali.

Katika kongamano hilo anatoa wito kwa walimu, wazazi, walezi na wanajamii kwa pamoja kuwa na utamaduni wa kusoma na watoto wao kwani watoto huiga kutoka kwao na hivyo kwa kuwapa fursa kutaimarisha mawasiliano zaidi kati yao na kuboresha stadi za KKK.

Kadhalika anapongeza juhudi za Shirika la Room to Read kwa kuandaa kongamano hilo ambalo linatoa fursa kwa wadau wa elimu na waandishi wa vitabu kupata muda wa kutoa maoni yatakayosaidia kupiga hatua katika kuboresha mazingira ya kusoma na kujifunza kwa maendeleo ya taifa.

Mkurugenzi Mkazi wa Room to Read Juvenalius Kuruletera, anasema shirika hilo kwa sasa linafanya kazi katika nchi 23 duniani na tano za Afrika ikiwamo Tanzania likijikita katika kuimarisha stadi za kusoma, tabia za kusoma na usawa wa kijinsia kwenye elimu.

Anasema shirika hilo linafanya kazi kwa kushirikiana na jamii iliyopo maeneo ya mradi lengo likiwa ni kukuza ujuzi wa kusoma na kuandika na kujenga tabia ya kupenda kusoma miongoni mwa watoto wa shule za msingi.

"Pia tuna mradi wa elimu kwa msichana ili kuwasaidia kumaliza shule za msingi na sekondari wakiwa na stadi muhimu zitakazowawezesha kufanya kwa kina maamuzi ya msingi ili wafanikiwe kimaisha," anaeleza.

Kuruletera anasema shirika hilo kupitia mradi wa usomaji na maktaba wanaamini kwamba maktaba ndiyo sehemu pekee ambayo mtoto anaweza kupata fursa ya kuendeleza stadi za KKK na kujenga tabia ya kujisomea.

"Room to Read tunamsaidia mtoto kumjengea msingi bora wa kumudu stadi za kusoma na kuandika kwa wakati katika ngazi za ya darasa lakwanza na la pili na kisha kutumia stadi hizo kujisomea kupitia vitabu vya hadithi kwenye maktaba," anasema.

> Serikali, wazazi na walezi, mashirika yasiyo ya kiserikali na jamii wanatakiwa kuwapa watoto fursa ya kujisomea vitabu vya hadithi wakiwa shuleni, nyumbani na mahali pengine ambapo ni salama.

"Ni muda wa serikali na wadau mbalimbali wa elimu kuanzisha maktaba kwenye shule zote za msingi ili vitabu viwekwe kwenye mpangilio maalumu na rafiki kwa watoto kuvifikia na kuazima na shirika letu tuko tayari kushirikiana na kutoa ushauri wa kiufundi katika kuendesha maktaba hizo," anasisitiza.

Anasema serikali, wazazi na walezi, mashirika yasiyo ya kiserikali na jamii wanatakiwa kuwapa watoto fursa ya kujisomea vitabu vya hadithi wakiwa shuleni, nyumbani na mahali pengine ambapo ni salama.

Mwalimu wa darasa la pili katika Shule ya Msingi Kibamba, Clotilda Shirima, anasema kwamba wepo wa maktaba shuleni umeamsha ari ya kusoma kwa watoto wengi ambao walikuwa hawana mwamko huo.

Shirika anasema hali ya usomaji awali haikuwa nzuri lakini baada ya kuanzishwa kwa maktaba wanafunzi wengi wamekuwa wakipenda kusoma mara kwa mara na wameanzisha utaratibu wa kuanzima vitabu na kwenda kujisomea nyumbani.

"Mwanafunzi akiwa hajui kusoma hana mwamko wa elimu lakini baada ya kuanza kwa maktaba shuleni kwetu imesaidia kuleta mabadiliko wengi sasa wanajua kusoma na wana ari ya kuazima vitabu kwenda kusomea nyumbani ambao hawajui kwa sasa ni wale watoro," anasema.

Mwalimu huyo pia anabainisha kwamba Shirika la Room to Read limetoa mafunzo ya kufundisha kwa walimu ambayo yamefanikisha kuwezesha kutamka herufi kwa sauti hatua ambayo imekuwa ni sababu wengi kujua kusoma na kuandika kwa haraka.

Mwalimu Eliamani Ayo anashukuru Shirika la Room to Read kwa kufanikisha kuwepo kwa maktaba shuleni lakini wingi wa vitabu vya hadithi ambavyo vinatosheleza wanafunzi kuazima na kwenda kujisomea nyumbani.

"Ujio wa shirika hili kwenye shule yetu imekuwa na faraja tumepata mbinu mpya ya ufundishaji ambayo hata baada ya mwalimu kufundisha wanafunzi wanajisomea wenyewe mmoja mmoja," anasema Ayo.

SAYANSI
NA MWANDISHI WETU

# Zijue mbinu za kuacha kuhaha kusaka usingizi mwororo usiku


Namna bora ya kulala inapendekezwa kutumia upande wa kushoto ili kuruhusu mfumo wa damu na michakato mwilini kufanyika kwa salama. **PICHA: MTANDAO**

WAPO wanaolala chali au kulalia mgongo, kifudifudi au kwa upande, bila mto au na mto, wengine wakipanga mito katikati na kuilalia ili kupata usingizi.

Hali inakuwa mbaya msimu wa joto kama ilivyo sasa. Lakini, swali linabaki ni njia gani bora za kulala usiku ili kupata usingizi mwororo usio na bughudha? Ikiwa unaishi kwenye eneo lililoathiriwa na joto unaweza kuishia kurukaruka na kugeuka geuka usiku kucha ukitafuta usingizi wa utulivu, usiupata kwa hiyo joto, kelele, wadudu kama mbu waweza kuwa maadui wakuu.

BBC Swahili inaeleza kuwa uchunguzi unaofanywa kupitia mabaharia wanaoendesha kazi zao zaidi majini hasa baharini, unaonyesha kuwa maeneo hayo yanaweza kuwa na manufaa kwa watu kupata usingizi wa itulivu usiku.

Chakula hicho ubongo au usingizi ni muhimu kwa maisha ya binadamu wote lakini inavyoelekea umefanyiwa utafiti kwa kiasi kidogo, BBC inasema. Watafiti wamejaribu mbinu tofauti, ikiwa ni pamoja na kuwarekodi watu wakiwa wamelala au kutumia teknolojia inayoweza kuvaliwa inayofuatilia mienendo yao usingizini lakini kazi zaidi inahitajika.

Watoto wadogo chini ya umri wa miaka mitatu wanalala kwa njia zaidi ya moja na kwa kawaida watoto hulala chali kwa sababu wanalazwa katika vitanda vyao vilivyopangwa ambavyo vimetandikwa kwa njia hiyo, ili kuwaweka salama na si kuanguka.

Kulala kwa ubavu ni nafasi ya kawaida ya kulalia, na watu wengi waliohojiwa wanachagua kama nafasi yao bora zaidi ya kulala. Utafiti huo unasema kwamba pande zote hazifanani, na wale waliolala upande wao wa kulia walilala kidogo zaidi na bora zaidi kuliko wale waliolalia mkono wa kushoto, na kufuatiwa na wale waliolala chali.

Mabaharia mara nyingi hulala kwa ubavu, wakisema kwamba sababu ni kwamba unaweza kupata usingizi wa haraka, kabla ya wengine kulala na kupunguza kukoroma. Utafiti mwingine mdogo ulifanywa kwa mabaharia wanaofanya kazi kwenye meli za kibiashara na kugundua kuwa matatizo ya kupumua kama vile kukoroma ni ya kawaida zaidi wakati mabaharia wanapolala chali.

Kwa hiyo jibu, hata hivyo, ni kwamba ikiwa unapambana na kiungulia, inafaa kujaribu kulala upande wako wa kushoto mara nyingi zaidi katika siku zijazo, ulalaji ambao ni nzuri kwako unasaidia pia kuweka tumbo sawa.

Shirika la Afya (WHO) linashauri chumba chako cha kulala kiwe na utulivu, chenye giza, kilichotulia na chenye joto au ubaridi unaostarehesha. Unashauriwa pia kuondoa vifaa vya kielektroniki vinavyoweza kuleta mwanga kama vile TV, kompyuta na simu za mkononi mahali unapolala.

Lakini ili ulale salama na kwa furaha acha kula milo mizito usiku, achana na vinywaji vyenye kafeini kama kahawa, pombe zikiwamo kali na mvinyo kabla ya kulala.

Inashauriwa kuwa watu wazima wanapaswa kulala saa saba au zaidi kwa usiku mara kwa mara ili kukuza afya bora. Kulala chini ya muda huo kila usiku kwa kawaida kunahatarisha afya, ikiwa ni pamoja na kunenepa kupita kiasi, kisukari, shinikizo la damu, maradhi ya moyo na kiharusi na hata kifo.

Upande unaopendekezwa kulalia ni wa kushoto. Lakini kuna angalizo, kutegemeana na masuala ya afya unayokabiliana nayo. Upande wa kushoto unaweza kukupa manufaa zaidi, hasa kwa wale ambao ni wajawazito au wenye tatizo ya kiungulia na gesi tumboni wanaweza kuwa waangalifu na upande wao wa kushoto.

Mtandao wa Sleep Foundation, unasema kuwa unapolalia tumbo lako, mwili wako huzama ndani ya godoro kwa sababu ya uzito wake.

Inawezekana ukaumwa mgongo, pengine unaweza kupinda na kuzisumbua pingili na hata shingo kwa vile itakuwa vigumu kuunyoosha kutokana na ukweli kuwa uko usingizini.

Mtandao unaongeza kuwa wakati mgongo wako hauko vizuri kwenye mpangilia wa maumbile unaweza kupata matatizo pengine pingili kuumia na kusababisha maumivu ya shingo, mabega na mgongo wakati wa kuamka.

Kulala kwa tumbo kunaweza pia kuongeza hatari yako ya maumivu ya shingo. Unapolalia tumbo lako, lazima ugeuze kichwa chako upande mmoja ili kupata hewa na kupumua kwa vile ukilalia uso unaziba pua na mdomo.

Kugeuza kichwa chako kunahitaji kugeuza shingo yako, ambayo huiondoa kutoka kwenye usawa na mgongo wako wote ikimaanisha unaipeleke kwingine kwa vile unaangalia pembeni.

Zaidi ya maumivu ya mgongo na shingo, mkao mbaya wa usingizi unaweza kusababisha matatizo ya ziada kama vile maumivu ya kichwa na bega au hata mkono wote.

Unaongeza makunyanzi usoni, ukijizoeza kulalia tumbo kwa sababu wakati upande mmoja wa uso wako umebanwa kwenye mto, hunyoosha, kuvuta, na kukandamiza ngozi yako na matokeo yake ni makunyanzi. Lakini kulalia tumbo lako kunaweza kuchangia kasoro za uso kuanzia kuvimba.

## Wanafunzi wanavyochefuka na vigodoro vimezidi kuaibisha

INATOKA UK.11

"Sina takwimu kamili za matukio, lakini ukweli ni kwamba vitendo vya ukatili vinafanyika katika shule za msingi, sekondari na nyumbani, tuungane kutoa elimu kuhusu madhara ya vitendo hivyo," anasema.

Mkurugenzi wa WAJIKI, Janeth Mawinza, anasema kwa muda mrefu shirika lake limekuwa likitoa elimu kuhusu madhara ya rushwa ya ngono kwa wanafunzi, katika wilaya ya Kinondoni na maeneo mengine ya Dar es Salaam ili kuwaepusha na ukatili wa kijinsia.

"Leo tumewaita katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kike Duniani, kwa lengo la kutaka kuunganisha nguvu za pamoja ikiwa ni mwendelezo wa kutaka kusaidiana kutoa elimu hii," anasema Janeth.

Anaongeza kuwa elimu kuhusu madhara ya rushwa ya ngono inahitajika, kwa kuwa bado mtoto wa kike anaendelea kukumbana na rushwa hiyo ambayo mwisho wake ni kumharibia maisha iwapo hatakuwa na uelewa wa kutosha wa kupambana nayo.

"Shirika letu linafanya kazi hii kwa kushirikiana na Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT)) na bado tunahitaji wafadhili zaidi kwani vitendo vya ukatili vipo na vinachangiwa na mambo mengi," anasema.

Mkurugenzi huyo anasema, wakati mwingine baadhi ya wazazi, walezi, watu wanaosimamia kesi za vitendo hivyo wasio waaminifu, wanachangia kufanya kesi ziishe kienyeji.

Anasema ni muhimu kuijengea jamii uelewa wa kutosha ili matukio ya ukatili kwa watoto wa kike yanapotokeza, wachukue hatua sahihi zza kukabiliana nayo bila kushawishiwa na kuyamaliza kienyeji.



# BAKWATA yawaomba viongozi wa dini kuombea uchaguzi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

BARAZA Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Wilaya ya Dodoma limewataka viongozi wa dini kuombea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika mwakani ili taifa lipate viongozi wanaowajali Watanzania.

Mwenyekiti wa baraza hilo, Bashiru Omary, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Alisema ni muhimu viongozi hao kuombea uchaguzi huo ili kupata watu wenye maadili na watakaosaidia serikali kuleta maendeleo kwa wananchi wake.

Aidha, Omary alisema viongozi hao wahakikishe wanashirikiana na serikali katika kulinda amani na kuhubiri upendo na mshikamano bila kuangalia itikadi ya kisiasa na ya kidini.

Alisema: "Jukumu la kuwapata vongozi wenye kuwajali Watanzania bila kuangalia itikadi za dini na vyama vya siasa na ambao wana hofu ya Mungu, jukumu hilo lipo mikononi mwetu kwa kushirikiana kwa pamoja kwa vitendo".

Kadhalika, aliziomba taasisi zote za dini ya kiislamu kujitoa kwa watu wenye kuhitaji mahitaji muhimu kama alivyokuwa akifanya Mtume kwenye maisha yake ya kuwajali watu.

# Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vyatakiwa kusimamia mitaala

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAKUU wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii nchini wametakiwa kusimamia mafunzo ya mitaala mipya iliyoboreshwa, ili kuleta matunda ya ajira kwa wahitimu wa vyuo hivyo.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsi, Wanawake na Makundi Maalumu, Amon Mpanju, alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akifunga mafunzo ya siku tatu kwa wahadhiri, wakufunzi na wakuu na makamu wakuu wa vyuo vya maendeleo nchini yaliyofanyika jijini hapa.

Mpanju aliwataka wakuu hao kwenda kusimamia mafunzo ya mitaala hiyo mipya ili kuzalisha wataalamu wenye ujuzi wa kujiajiri na kuajiri wengine.

"Nimeambiwa mmepata mafunzo hayo kwa muda wa siku tatu hivyo nawataka mkasimamie vizuri mitaala hii mpya iliyoboreshwa ili kuzalisha wataalamu wenye ujuzi wa kisasa wa kuweza kujiajiri," alisema.

Kadhalika alisema lengo la kufanyika kwa mapitio ya mitaala hiyo ni kuhakikisha wanakuwa na masomo wenye uwezo wa kuwajenga wahitimu wa vyuo hivyo kuwa na uwezo wa kuzalisha wataalamu bora.

Pia aliwataka kutunga mitihani na majaribio ya upimaji unaozingatia miongozo na mitaala hiyo mipya ili kuongeza watu wenye ujuzi zaidi.

Mratibu Mkuu wa Mitaala Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET), Dk. Edward Mneda, alisema maboresho ya mitaala hiyo yalianza mwaka jana kwa kushirikisha wataalamu kutoka vyuo vya maendeleo ya jamii nchini.

Dk. Mneda alisema kwa mujibu wa sheria inawataka kufanya maboresho ya mitaala ya kujifunza na kufundishia kila baada ya miaka mitano na iliyokuwepo imeisha muda wake Juni mwaka huu na mitaala hiyo iliyozinduliwa jana inatarajiwa kutumika hadi mwaka 2027.

Alibainisha kuwa mitaala hiyo iliyozinduliwa itasaidia kuondoa matatizo ya ajira na kuboresha uwezo wa wahitimu wa vyuo hivyo kuingia kwenye soko la ajira kitaifa na kimataifa.

Alisema mitaala hiyo inamjenga kijana kujitegemea na kuwajengea umahiri katika na kuzijengea tasisi hizo kuwa na vijana wenye mbinu za kisasa za kujifunza.




Daktari wa Macho, Dk. Edmund Malinzi, kutoka Hospitali ya CCBRT akimhudumia mmoja wa wananchi waliofika kupata huduma katika banda nje ya hospitali hiyo, Msasani, Dar es Salaam jana, ikiwa ni maadhimisho ya Siku ya Afya ya Macho Duniani, CCBRT kwa kushirikiana na wadau wake Square Pharmaceuticals LTD wametoa huduma ya upimaji afya ya macho na dawa bila malipo kwa wananchi wa Msasani na maeneo ya jirani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yatoa maagizo kwa vituo vya kulea watoto yatima

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imevitaka vituo vya kulelea watoto yatima na wenye mahitaji maalum kuacha kuvitumia kama vyanzo vyao vya mapato, badala yake watumie kuwapa malezi bora watoto.

Kaimu Kamishna wa Ustawi wa Jamii kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Tulo Masanja, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki kwenye kumbukizi ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere jijini hapa.

Alisema vituo vingi vimekuwa vikitumia vituo kama vyanzo vya mapato, suala ambalo halikubaliki na kama kuna kituo chochote kinafanya hivyo kinapaswa kuachwa mara moja.

"Tunaomba vituo hivyo vitumie misaada vinayopewa kwa manufaa ya watoto na siyo vinginevyo, kwa sababu jamii inatoa msaada kwa lengo la kuhakikisha watoto hao wanapata mahitaji kama watoto wengine," alisema Masanja.

Naye Katibu wa Dawati la Jinsia kutoka Jeshi la Magereza, Scholastica Ndunguru, alisema wameamua kuadhimisha kumbukizi ya Baba wa Taifa kwa kutoa misaada mbalimbali kwa watoto wenye uhitaji maalum kutoka baadhi ya vituo vya kulelea watoto yatima na wenye uhitaji.

Ndunguru alisema mpango huo utakuwa endelevu hasa ukizingatia watoto wanahitaji kutunzwa ili kutimiza ndoto zao.

Mkuu wa Kitengo cha Ustawi wa Jamii kutoka Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, Elvira Mutagwaba, alizitaka taasisi zingine kuiga mfano wa Jeshi la Magereza kutoa msaada kwa watoto wenye uhitaji maalum ili kupata elimu ambayo itawasaidia hapo baadaye.

Alisema wana watoto wengi wenye mahitaji maalum, hivyo taasisi nyingine zikijitoa zitakuwa zimesaidia kwa kiasi kikubwa kuwainua watoto hao kiafya pamoja na kielimu.

# Washauri wanaojiunga darasa la kwanza wapimwe afya

**Na Paul Mabeja,** CHAMWINO

SERIKALI imeombwa kuweka utaratibu wa kupima afya za watoto wanaoandikishwa kujiunga darasa la kwanza nchini ili kuwatambua mapema wenye ulemavu na kuwapatia mahitaji kwa mujibu wa hali zao.

Meneja miradi wa shirika linalojihusisha na masuala ya watu wenye ulemavu la Foundation For Disabilities Hope (FDH) Johnson Mbwambo, alisema hayo jana wakati akikabidhi misaada ya vitu mbalimbali kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Buigiri wasioona.

Mbwambo, alisema ipo haja kwa serikali kuweka utaratibu wa kupima afya kwa watoto wote wanaoandikishwa kujiunga darasa la kwanza ili kutambua afya zao.

"Serikali iweke utaratibu wa kupima afya watoto wote wanaojiunga darasa la kwanza ili kutambua wenye ulemavu mapema hali ambayo itasaidia kupata mahitaji kulingana na hali zao," alisema.

Kadhlika, alisema ipo haja kwa serikali kuwekeza kwenye kuandaa walimu wengi wa elimu maalum ili kukidhi mahitaji yaliyopo nchini.

"Rai yangu serikali iongeze idadi ya walimu wa mahitaji maalum nchini kwa kuwa mtoto mwenye mahitaji maalum kufundishwa na mwalimu wa kawaida anaweza asielewe lakini wenye taaluma ya elimu maalum anaweza mwelewa mtoto kama ana uoni hafifu au usikivu hafifu," alisema.

Kadhalika, aliiomba serikali kuendelea kuboresha miundombinu ya shule ili kuwezesha watoto wenye ulemavu kupata elimu katika mazingira rafiki.

Ofisa Programu Jinsia, Wanawake, Vijana na Watoto wa shirika hilo, Halima Msofe, alisema jamii inapaswa kushirikiana kwa pamoja kutatua kero mbalimbali wanazokumbana nazo watoto wa kike hasa wenye ulemavu.

"Jamii inapaswa kushirikiana kwa pamoja kutatua changamoto za watoto wa kike na kuwapa msaada wanapohitaji lakini pia watoto wa kike wanaowajibu wa kujitambua na kusoma kwa bidii ili kufikia ndoto zao," alisema Msofe.

Vile vile, alisema misaada waliyotoa kwa watoto hao ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Kike Duniani.



# Wananchi walia na ongezeko la nauli Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI mkoani Mbeya wamewalalamikia baadhi ya wamiliki wa magari ya abiria kupandisha nauli holela kwa kisingizio cha kupanda kwa bei ya mafuta, wakidai kuwa kitendo hicho kinawaongezea ukali wa maisha.

Hivyo, wameiomba serikali kuingilia kati kwa kudhibiti ongezeko hilo la nauli wakieleza kuwa hakuna mahali waliposikia serikali ikitangaza nauli mpya, lakini wanatozwa na makondakta wa magari huku wengine wakitumia nguvu.

Walitoa kilio hicho mwishoni mwa wiki walipozungumza na Nipashe kwenye vituo mbalimbali vya daladala na mabasi ya kwenda mikoa jirani, ambapo walisema ni wiki sasa wanatozwa nauli kubwa lakini hakuna kauli yoyote ya serikali iliyotolewa.

Mmoja wa wananchi hao, Joseph Mwamwezi, alisema kutoka katika Mji Mdogo wa Mbalizi kwenda Stendi Kuu mpaka Sokomatola jijini Mbeya walikuwa wanatozwa Sh. 550 lakini kwa sasa wanatozwa Sh. 700.

Alisema kutoka Mbalizi kwenda Uyole walikuwa wanalipa Sh. 1,000 lakini kwa sasa wanatozwa Sh. 1,400 na kwamba haifahamiki kanuni iliyotumika kupandisha nauli hizo.

"Tunaiomba serikali ikae na wamiliki wa magari ili tuijuwe nauli halisi ambayo tunatakiwa kulipa, kwenye daladala zote za kwenda Sokomatola imeandikwa nauli ni Sh. 550 na hata Sh.500 walikuwa wanapokea lakini sasa hivi ni wiki inaelekea kukamilika tunatozwa Sh.700," alisema Mwamwezi.

Naye Paulina John ambaye ni mkazi wa Mpemba mkoani Songwe alisema nauli ya kutoka Mbeya Mjini kwenda Tunduma walikuwa wanatozwa Sh. 5,000 lakini kwa sasa wanatozwa Sh. 6,000 bila kupewa tiketi kwa kisingizio kwamba bado hazijaandaliwa.

Aliiomba serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu (LATRA) kuweka wazi kama kuna nauli mpya zimetangazwa ili zibandikwe kwenye magari kuepuka migogoro kati ya abiria na makondakta wa magari hayo.

"Tunaomba serikali iwe inawahi kutoa majibu kwa sababu tunaumia, unajikuta unashida ya kusafiri na umeandaa nauli yako bila kujua kwamba kuna mabadiliko ya nauli unakutana na makondakta wanakutangazia kabla hujapanda gari kwamba kuna ongezeko la nauli na wanakutaka kama hauko tayari usipande," alisema Paulina.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon Mayeka, aliwapiga marufuku makondakta wa mabasi yanayosafirisha abiria kutoka Mbeya Mjini kwenda wilayani humo kupandisha nauli mpaka watakapotangaziwa na serikali.

Alisema yeyote atakayebainika kupandisha nauli atachukuliwa hatua kali za kisheria ili iwe fundisho kwa wengine kwa maelezo kuwa upo utaratibu maalumu wa kupandisha ama kushusha nauli kwenye vyombo vya usafiri.

Ofisa Mfawidhi wa LATRA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Omary Ayoub, alisema wameshaanza kuchukua hatua kwa wamiliki wa mabasi ambao wamepandisha nauli kiholela ikiwa ni pamoja na kuwatoza faini.

Alisema mpaka sasa baadhi ya mabasi ya kwenda Chunya pamoja na daladala zinazofanya kazi katikati ya Jiji la Mbeya zimetozwa faini ya kati ya Sh. 250,000 mpaka Sh. 300,000 kutokana na kutoza nauli kubwa kwa abiria.

Aliagiza mabasi yote kuhakikisha yanatoa tiketi halali kwa abiria huku akiwataka abiria kuhakikisha wanatunza tiketi hizo kama ushahidi na kuziwasilisha kwenye ofisi za mamlaka hiyo ili hatua zichukuliwe.



Baadhi ya abiria wakiwa wamekwama katika stendi ya mabasi ya Tarafani Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi jana kutokana na mgomo wa daladala zinazofanya safari zake katikati ya Jiji la Mbeya na wilayani. **PICHA NA NEBART MSOKWA**

# Wakazi 100,000 wa Njombe wakosa huduma ya majisafi

**Na Elizabeth John,** WANGING'OMBE

WAKAZI zaidi ya 100,000 kutoka Tarafa ya Wanging'ombe mkoani Njombe wanakosa huduma ya majisafi kutokana na baadhi ya wakulima wa vijiji vya Mngate na Imalinyi kuzuia chanzo cha maji cha Mto Mbukwa na kuyatumia katika shughuli za umwagiliaji wa mazao.

Hayo yalibainika juzi wakati wa operesheni maalumu iliyofanywa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Wanging'ombe na kubaini ekari 10 za vitunguu zimelimwa karibu na chanzo cha maji, huku maji yakiwa yamezuiwa na kuelekezwa shambani.

Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe, Claudia Kitta, alisema kuwa watawachukulia hatua kali wakulima wote wanaotumia maji ya mito kuyachepusha kwenye mifereji yake na kuyapeleka kwenye mashamba yao.

"Hii operesheni ndio kwanza imeanza kwa wote wanaonisikia hata kwenye vyanzo vingine. Sio eneo hili tu, tuna vyanzo vingi katika maeneo mbalimbali shughuli kama hizi yaelekea zinafanyika," alisema Kitta.

Kitta aliwataka wananchi kuzingatia sheria na kuacha tabia ya kulima kwenye vyanzo vya maji.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Wilaya ya Wanging'ombe (WANGIWASA), Mhandisi Emanuel Konkomo, alisema kilimo kinachofanyika kwenye vyanzo vya maji ndani ya mita 60 kina madhara makubwa kwa binadamu.

"Kwanza maji ya mto yanapohamishwa kuelekea kwenye mashamba wananchi kule wanakosa maji maana yake shughuli nyingi za uchumi kwa watu kama 100,000 zinasimama wanaanza kutafuta maji," alisema.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mngate, Shabani Fute, alisema wanafanya mikutano mbalimbali ya kuelimisha wananchi kuacha kulima kwenye vyanzo vya maji lakini kuna baadhi ya wakulima ambao bado wanakiuka.

# Katibu Mkuu Ardhi aipiga 'tafu' shule ya sekondari

**Na Elizabeth John,** MAKETE

KATIBU Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Antony Sanga, amekabidhi vitabu vya kiada vya Sh. milioni saba katika Shule ya Sekondari Lupila wilayani hapa.

Sanga alikabidhi vitabu hivyo katika mahafali ya 32 ya kidato cha nne shuleni hapo, ambapo aliwataka walimu na wanafunzi kuvitumia vitabu hivyo ili kupandisha taaluma.

"Vitabu vyote sasa viko hapo na vyote mlivyoviomba tumewaletea, walimu mnapaswa kuvitumia na wanafunzi msome kwa bidii kwa sababu hakuna kisingizio tena," alisema Sanga.

Sanga alisema vitabu hivyo vimetolewa na Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) kwa niaba ya wadau wengine wa maendeleo katika Wilaya ya Makete.

Akizungumzia kuhusu changamoto ya umeme kutofika katika shule hiyo alisema wataendelea kulishughulikia suala hilo sambamba na changamoto ya Barabara ya Lupila hadi Kipengele ili kuwapunguzia adha wananchi wa ukanda huo hasa wanafunzi.

Mwenyekiti wa bodi ya shule hiyo, Daniel Okoka, aliwapongeza wadau wa maendeleo pamoja na serikali kwa mchango wao katika kutatua changamoto shuleni hapo.

Mkuu wa shule hiyo, Abkasa Ngwale alisema kutatuliwa kwa changamoto ya vitabu itasaidia kuwaongezea ufanisi kwenye ufundishaji ukilinganisha na hapo awali.

"Kutatuliwa kwa changamoto hii ya vitabu ni fursa kwetu sisi walimu kufundisha kwa ufanisi ili wanafunzi waweze kufaulu," alisema Ngwale.

**Sanga alisema vitabu hivyo vimetolewa na Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) kwa niaba ya wadau wengine wa maendeleo katika Wilaya ya Makete.**



# Polisi yakamata watuhumiwa wizi, utapeli, umiliki silaha

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JESHI la Polisi Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, linawashikilia watuhumiwa mbalimbali kwa makosa ya wizi, utapeli na umiliki wa silaha kinyume na sheria.

Kati ya wanaotuhumiwa hao wapo vijana wawili wenye umri wa miaka 18 ambao wanashikiliwa kwa makosa ya kumiliki silaha na wizi.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, Richard Thadei Mchomvu, alisema watuhumiwa hao kwa nyakati tofauti wamekamatwa katika mkoa huo ambapo Khelef Khamis Abeid miaka 18 mkaazi wa Bububu Kijichi amekutwa na bastola aina ya rietro bereta yenye namba 69085 ikiwa na risasi tano.

Alisema Agosti 30 mwaka huu majira ya saa 1:00 usiku maeneo ya Forodhani mtuhumiwa huyo alikutwa na bastola hiyo na baadaye alikwenda kupekuliwa nyumbani kwake na kupatikana na risasi moja ikiwa juu ya kabati kwenye chumba anacholala.

Kamanda Mchomvu alimtaja mtuhumiwa mwingine kuwa ni Expeling Amara Projestus (18) mkazi wa Amani anashikiliwa kwa kosa la wizi ambapo alikamatwa katika Hosptali ya Rufani Mnazimmoja akiwa amevaa nguo ya daktari na kupita kwenye vyumba vya wagojwa na kuwaibia vitu mbalimbali ikiwamo simu.

Alisema pia wamefanikiwa kuwakamata watuhumiwa Haji Abdalla Haji, Ali Mohd Ali wakiwa na madumu 55 ya mafuta ya dizeli ambayo yanatuhumiwa kuwa ya wizi na Maruani Soud Abdalla (22) mkazi wa Mchangani kwa kosa la wizi na kukutwa na kompyuta.

Kadhalika, alisema Jeshi la Polisi limewakamata watuhumiwa wawili sugu ambao ni Iddi Kigoda Iddi (37) mkazi wa Kwamchina na Ramadhan Mohammed Salum mkaazi wa Tomondo visiwani humo.

Alisema watuhumiwa hao wamekuwa wakiendesha vitendo vya utapeli kwa kujifanya madalali na wamiliki wa nyumba, kwamba kuwakodisha wananchi kwa kuwaibia fedha na hatimaye kukimbilia eneo la Pujini kisiwani Pemba.

Kamanda Mchomvu alisema baada ya polisi kupata taarifa hizo walifanikiwa kuwakamata watuhumiwa hao wakiwa wamejificha katike eneo hilo.

Kadhalika, alisema wamefanikiwa kukamata simu 58, runinga, pikipiki yenye namba za usajili Z.903 LR, kishkwambi, baskeli moja na mkoba mmoja wa kike rangi ya kijivu.

Alisema hatua hiyo imefikiwa kutokana na ushirikiano mzuri uliopo kati wananchi na vyombo vingine vya ulinzi na usalama na jeshi hilo.

Hivyo aliwaomba wananchi kuendelea kushirikiana na jeshi hilo na kuwafichua wahalifu ili kuona wanakamatwa na kuchukuliwa hatua.

Pia, aliwashauri wananchi kuhakikisha wanashirikiana na masheha katika shehia zao pale wanapotaka kununua nyumba, kiwanja au vitu vyengine vya thamani ili kuepuka kutapeliwa.

# Bei ya karafuu Zanzibar yafikia 15,000/- kwa kilo

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imeongeza bei ya karafuu kwa wakulima kutoka Sh.14,000 hadi Sh.15,000 kwa kilo.

Hivyo, imewataka wakulima wa zao hilo kutumia majamvi kwa ajili ya kuanika mazao yao ili kufikia ubora wa viwango vitakavyoingia katika soko la dunia.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa Mfuko wa Barabara, Ali Suleiman Mussa, wakati akizungumza na wakulima wa karafuu eneo la Matemwe Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema katika kufikia ubora utakaoziingiza karafuu za Zanzibar katika soko la kimataifa zinatakiwa kuanika kwa kutumia majamvi.

Alisema kitendo cha kuanika karafuu sakafuni au barabarani ni sawa na kuzishusha thamani ya ubora wake ambapo serikali itashindwa kupata kiwango cha juu cha daraja la kwanza katika soko la dunia.

Alisema Shirika la Taifa la Biashara kwa nyakati tofauti limetoa vifaa vya kuanika karafuu ikiwamo majamvi kwa wakulima kwa lengo la kuvitumia ili kufikia kiwango cha daraja la kwanza.

Ofisa Ununuzi wa Karafuu kutoka Kituo cha Donge Wilaya ya Kaskazini Unguja, Haji Faki Ali, alisema baadhi ya karafuu zinazofikishwa hapo na kupimwa hazijafikia kiwango cha daraja la kwanza kwa sababu ya kukosa vifaa rasmi vya kuanikia karafuu ambavyo ni majamvi.

Alisema karafuu ambazo zitaanikwa chini ikiwamo barabarani zinapoteza ubora wake kufikia kiwango cha daraja la kwanza pamoja na kuwa na mchanganyiko mwingi wa mchanga.

"Wakulima wakati wanapoanika karafuu zao watumie vifaa rasmi vinavyokubalika ambavyo ni majamvi pamoja na mikeka kwa ajili ya kupata kiwango cha daraja la juu," alisema.

Baadhi ya wakulima wa karafuu waliliomba Shirika la Taifa la Biashara kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu kutoa mikopo zaidi ambayo itawawezesha kununua vifaa vitakavyotumika kwa ajili ya kuanika karafuu.



Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman (kushoto), akiwa na mwakilishi wa Jimbo la Tumbatu, Haji Omar Kheri, katika Maulid iliyofanyika kisiwa cha Tumbatu Mkoa wa Kaskazini Unguja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yazihakikishia asasi mazingira rafiki ufanyaji kazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MRAJISI wa asasi za kiraia Zanzibar, Ahmed Khalid Abdullah, amesema serikali itaendelea kutayarisha mazingira mazuri kwa ajili ya asasi za kiraia kufanya kazi zao kwa sababu zinamchango mkubwa katika kusaidia miradi ya kijamii.

Aliyasema hayo jana wakati wa hafla ya uzinduzi wa mradi wa majaribio wa vichujio vya maji ambao utahusisha Shehia ya Kisauni, Chukwani na Welezo.

Mradi huo unatekelezwa na Kanisa la Pentecostal Evangelistic Fellowship of Afrika (PEFA) lililopo Kisauni chini ya ufadhili wa mradi wa Watchmen International kutoka Marekani.

Alisema serikali inajitahidi kuhakikisha wananchi wanaishi kwa kupata huduma ya majisafi na salama, hivyo mradi huo umekuja muda mwafaka katika kulinda afya za wananchi.

Alisema lazima kuwe na teknolojia ya kukinga maradhi mbalimbali katika matumizi ya maji, kwa sababu maji ni uhai na kila mmoja anaumuhimu wa kutumia huduma hiyo ya maji.

"Tunaelekea katika kipindi cha mvua kubwa na sote mashahidi kwamba tuna sababu na kila njia ya kujikinga katika maradhi mbalimbali ambayo yanaweza kutokea katika kipindi cha mvua," alisema.

Mrajis huyo alisema dini zisaidie kujenga umoja, mshikamano na kuleta maelewano kwa wananchi wote bila ya kujali itikadi za dini, siasa wala kabila.

"Tujaribu kutumia dini zetu kuleta mshikamano, umoja, maelewano na mashirikiano, tunafahamu Zanzibar tunadini tofauti lakini tuchukue juhudi za makusudi kuona kwamba tunaondosha migogoro katika dini na ibada na hatimaye kushirikiana kwa pamoja ili wananchi kufanya ibada kwa amani na mshikamano," alisema.

Hivyo, aliwataka walengwa wa mradi huo kuwa mabalozi wa kutunza afya za wananchi kwa sababu kupata maradhi mbalimbali yanayotokana na maji ni sawa na kuhatarisha maisha ya wananchi.

Mkurugenzi wa mradi huo, Roger London, alisema kwa miaka 12 kampuni yake inafanya kazi katika maeneo mbalimbali na sasa imeamua kuleta mradi wa majisafi na salama Zanzibar kusaidia jamii kubaki salama.

Alisema duniani kote takwimu zinaonesha watoto 5,000 wanafariki dunia kutokana na kushindwa kunywa majisafi na salama, hivyo mradi huo unakwenda kuokoa maisha ya wananchi wakiwamo watoto.

Naye Mchungaji wa Kanisa la PEFA Zanzibar, Dk. Daniel Kwilemba, alisema vichujio vya maji vina uhitaji mkubwa Zanzibar kwa lengo la kuepusha maradhi ya mlipuko ikiwamo kipindupindu.

Aidha, alisema mradi huo ni wa majaribio, utaanza shehia tatu ambazo ni Chukwani, Kisauni na Welezo, ambapo baada ya matumizi ya majaribio watafanya tathmini kuangalia maeneo mengine kuendelea kuwapatia vichujio vya maji.

Alizishauri asasi zisizo za serikali kushirikiana na serikali katika maeneo muhimu ya jamii ikiwemo elimu na afya za wananchi kwa lengo la kupata maendeleo nchini.

Baadhi ya wananchi waliokabidhiwa vichujio vya maji, walisema si vyema jamii kudharau ili kujiepusha na maradhi, pia vifaa hivyo vitasaidia kupunguza gharama kwa serikali kununua dawa za maji.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE
Kituo cha JUMUISHI
Mkoa DAR ES SALAAM
Usimamizi wa mirathi Na 1545/2023
KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA
MAREHEMU DICKSON MASHAURI MFINANGA WA............
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA
NA MICHAEL DICKSON THUGO
ANGELA DICKSON MFINANGA
**TANGAZO**
(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, Wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 02 Mwezi 11 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani Kukaguliwa.

**Imetolewa leo tarehe 13 mwezi 10 Mwaka 2023**

HAKIMU

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**IRENE EZEKIEL NICHOLAUS** anatangaza kupotelewa na Passport yake yenye namba TAE485872 iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Makao Makuu tarehe 20/06/2022. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: PHQ/DAR/UBU/25884/2023.

## KUPOTEA KWA KADI YA GAJAJI

**JALI CHRISTIAN MLOWE**
anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji yenye namba za usajili MC 710 BPY aina ya TVS KING yenye Chassis namba MD6M14PK4G4L50434. Engine namba OK4LG4068068. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi:
**MKO/RB/2023.**

## KUPOTELEWA NYARAKA UMILIKI KIWANJA

**MAKAME KHAMIS SALUM**
anatangaza kupotelewa na nyaraka ya umiliki wa kiwanja namba 157 Kitalu "TT" kilichopo Butengwa Manispaa ya Shinyanga.
Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi:
**RB/MD/P25/VOL.VU/2023.**

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**BEN LEONARD MWAMBELA** anatangaza kupotea kwa hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba TAE 402117 iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 05/05/2021. Tarehe ya kuisha matumizi ni 04/05/2031. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/UBU/23029/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI TRAILER

RASHVIR SINGH GAHIR anatangaza kupotea kwa kadi za gari aina ya trailer zenye jina la umiliki TANGANYIKA UNIVERSAL TRANSPORT LTD. zenye usajili namba T 882 AME na CHASSIS NAMBA: JSSC1213947 na T 705 AFY na CHASSIS NAMB: STC12005PT013. Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
PHQ/ARU/ARU/4457/2023

## KUPOTEA KWA KADI GARI

RASHVIR SINGH GAHIR anatanagaza kupotea kwa kadi ya gari YORK FLAT BED yenye usajili namba T 683 AAG, CHASSIS NAMBA: A012396 na ENGINE NAMBA: 0000. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
PHQ/ARU/ARU/4458/2023

## CHETI KIMEPOTEA



**ANNASTAZIA JAMES LUKAMATA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number S5168/0004 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MOUNT MORIE SEKONDARI mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DOD/DOD/5337/2023.**

IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO
DISTRICT AT MOROGORO
PROBATE AND ADMINISTRATION
CAUSE NO. 106 OF 2023
In the Matter of the late: LUCIAN ADOLF PEMBE

**By 1. JULIANA DAUDI MKUMBO**
**2 ............................................**

ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above- named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the **19th October 2023.**
**Dated at Morogoro this 12th day of October 2023.**

RESIDENT MAGISTRATE


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EMMANUEL ARISTARICK SANGAWE**
Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina **PRADO** yenye namba za usajili namba **T826 ABK**
Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**POLISI TAARIFA :**
**ARU/ARU/RB/238406/2023**

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
DEED (MADE UNDER S. 10 OF THE OATHS (JUDICIAL PROCEEDINGS) AND STATUTORY DECLARATIONS ACT, CAP 34(R.E...2019)

This change of name deed is made on 5th day of October 2023 by me EMMANUEL SIXTUS MWINUKA formerly known as EMMANUEL SIXTUS BERNARD of MOROGORO. WITNESS AND HEREBY DECLARED AS FOLLOWS;

- I ABSOLUTE RENOUNCE AND ABANDON the use of other name of as EMMANUEL SIXTUS MWINUKA and EMMANUEL SIXTUS BERNARD and I assume and determine to take and use the new name EMMANUEL SIXTUS MWINUKA in substitution of my former names of EMMANUEL SIXTUS BERNARD.
- AND IN PURUANCE of such change of my names as aforesaid I DECLARE I shall at all times hereafter in all records , documents and other writings and in all action and dealings and on all occasions whatsoever use the new name of EMMANUEL SIXTUS MWINUKA in substitution for my former names of as EMMANUEL SIXTUS BERNARD.
- So relinquished as a foresaid former names but by the new name of EMMANUEL SIXTUS MWINUKA AND HEREBY AUTHORISE AND REQUIRE all persons at all times to describe and address me by the new name EMMANUEL SIXTUS MWINUKA
- What is stated hereinabove paragraphs 1, 2, 3 and 4, and is true to the best of my own knowledge and in accordance with The Oaths and Statutory Declaration Act, Cap 34 R.E 2019.



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MUFINDI
Kituo cha MAFINGA Mkoa IRINGA
Shauri la madai Na.36/2023
Jina la mdai MUCOBA BANK PLC
Jina la mdaiwa MSAMI ELIAS SHEDEWA
KUITWA SHAURINI MDAIWA
(kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)
Kwa MSAMI ELIAS SHEDEWA
Kwa kuwa mdai ameleta madai yake/yao kwamba ( eleza hapa habari za madai)

LILIKOPESHWA FEDHA TSHS. 12,811,295.50/= AMBAZO HUJAREJESHA kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 24 mwezi 10 mwaka 2023 saa 8:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.
ANGALIZO: kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 16 mwezi 10 mwaka 2023

IN THE JUVENILE COURT OF DAR ES SALAAM
AT KISUTU
JUVENILE CIVIL APPLICATION CASE NO 476 OF 2023
DOROTHY JOHN KIRIGITI MWITA ... APPLICANT
VERSUS
ODDO KOMBA KAMBE KAMBEKETA... RESPONDENT
NOTICE OF DATE O F HEARING / MENTION / JUDGMENT / RULING

**TAKE NOTICE** that, the above mentioned casehas been fixed fer hearing /mention / judgment / Ruling on the 18/10/2023 At 7.39AM.
**YOU** are requared to appear in this Court without fail and must produce on that day all the documents upon which you intend to relay in support of your case.
Given under my hand and the SEAL of the Court this 12 day of 10 2023

PRINCIPAL / SENIOR RESIDENT MAGISTRATE / RM
KISUTU – DAR ES SALAAM

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 136 OF 2023
In the matter of the Estate of the late SAMSON MAGAYO of Chalinze - Chamwino within Dodoma City
AND
In the matter of application for letters of administration
GEORGE SAMSON MAGAYO
GENERAL CITATION
(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above- named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above- named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 10 Day of November,2023
**Dated at Dodoma this 13 Day of October, 2023**

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**GODFREY EMANUELY LUTONJA**
anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili MC 504 DBU aina ya SAN LG. CHASIS NO; LBRSPJB56M9012585. NAMBA YA INJINI; SL157FM121914366. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA JESHI LA POLISI NAMBARI (LOSE REPORT) **PHQ/GEI/GEI/1163/2023.**

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 133 OF 2023
In the matter of the Estate of the late
SYLIVATUS BERATI KASHAGA
AND
IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY
SELINA WAYIMBA
GENERAL CITATION

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above- named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above- named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 2nd Day of November,2023
Dated at Dodoma this 09th Day of October, 2023

RESIDENT MAGISTRATE

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

## Kansela Ujerumani kuzuru Israel

**BERLIN,** Ujerumani

VYOMBO vya habari nchini Ujerumani vimeripoti kuwa kansela wa taifa hilo, Olaf Scholz, atasafiri kuelekea nchini Israel leo ikiwa ni sehemu ya kuonyesha mshikamano na taifa hilo kutokana na shambulio la wapiganaji wa Hamas.



Inaelezwa kuwa hiyo itakuwa ziara ya kwanza ya kiongozi wa nchi hiyo nchini Israel tangu kutekelezwa kwa shambulio la wapiganaji wa Hamas dhidi ya nchi hiyo.

Scholz aliahidi kuiunga mkono Israel katika mapambano yake na wapiganaji wa Hamas.

Hatima ya raia wa Ujerumani waliotekwa katika mapigano yao yanayoingia siku ya 10, imetajwa kuwa mojawapo ya agenda kuu ya mazungumzo kati ya kiongozi huyo na utawala wa Israel.

Ilielezwa kuwa Waziri wa Mambo ya kigeni wa Ujerumani, Annalena Baerbock, tayari yuko nchini Israel baada ya kuwasili wiki iliyopita.

Katika kikao cha wanahabari na mwenyeji wake wa Israel, Baerbock alilaani kile alichosema kwamba ni wapiganaji wa Hamas kuwatumia watoto kama kinga kwenye vita. **RFI**

# Uganda, DRC zakubaliana wananchi kusafiri bila visa

**KAMPALA,** Uganda

TAIFA la Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) zimekubaliana kuondoa masharti ya visa ili kuwawezesha raia wa mataifa hayo mawili kusafiri bila pasi hiyo ya kusafiria.

Kwa mujibu wa pande zote, makubaliano hayo yanalenga kurahisisha harakati za watu na kuimarisha biashara kati ya nchi hizo mbili.

Makubaliano hayo yanafuatia mazungumzo ya hivi karibuni kati ya maofisa wa nchi hizo mbili katika mji mkuu wa DRC, Kinshasa.

Rais wa Uganda, Yoweri Museveni kwa miezi kadhaa amekuwa akitetea uingiaji wa visa bila malipo kati ya nchi hizo mbili.

"Kuvuka katika Afrika Mashariki kunapaswa kuwa bila gharama. Unalipa visa unapoenda Marekani au Ulaya, lakini visa ya DRC, hiyo ni takataka. Ikiwa ni hivyo, nimeiondoa," Rais Museveni alisema Desemba mwaka jana alipozindua kituo cha mpakani cha Mpondwe kwenye mpaka wa Uganda na DRC.

Mwezi Mei, mwaka huu kiongozi huyo alitoa wito kwa maofisa kutoka nchi zote mbili kuharakisha mchakato wa kuanzisha usafiri bila visa.

Maraia wa Uganda na DRCongo hapo awali wamelalamika kuhusu kulipa ada kubwa ya visa katika vivuko vya mpakani. **BBC**



Miongoni mwa safari hatarishi za majini huko nchini DRC.. **PICHA: MTANDAO**

# UN: Mzozo wa Israel na Hamas umefikia pabaya

**NEW YORK,** Marekani

UMOJA wa Mataifa (UN) umesema mzozo kati ya Israel na Hamas umefikia hatua mbaya wakati hospitali za Gaza zikikaribia kuishiwa hakiba ya nishati na juhudi za kupitisha misaada ya kiutu katika mpaka wa Rafah zikiendelea.

Katibu Mkuu wa umoja huo, Antonio Guterres, alitoa wito kwa kundi la Hamas kuwaachilie huru mateka, huku ukiitaka Israel kuruhusu misaada ifike katika Ukanda wa Gaza.

Guterres alisema UN ina chakula, maji, dawa na mafuta ambayo tayari yako Misri na katika ukingo wa magharibi kwa ajili ya kupelekwa Gaza kama wafanyakazi wake wataruhusiwa kuvisafirisha bila ya vikwazo.

Guterres alitoa kauli hiyo wakati ambao zaidi ya watu milioni moja wamelazimika kuyahama makazi yao huku Israel ikitarajiwa kufanya uvamizi unaolenga kuliangamiza kundi la Hamas, lililovamia kusini mwa Israel zaidi ya wiki moja iliyopita.

Pia wito huo umetolewa wakati mashirika ya misaada ya kiutu yakifanya juhudi za kuingiza misaada Gaza katika mzozo ambao umesababisha vifo vya zaidi ya Wapalestina 2,600.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani imevinukuu vyombo vya habari vya Misri vilivyoripoti kuwa huenda mpaka wa Rafah kuingia Gaza ukafunguliwa kwa muda.

Awali shirika la habari la Reuters liliripoti likivinukuu vyanzo vya kiusalama vya Misri ambavyo halikuvitaja vikidai kuwa kungekuwa na usitishaji mapigano jana kuanzia saa tatu asubuhi suala ambalo pande zote mbili za mzozo zimekanusha.

Taarifa ya Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, ilisema kuwa kwa sasa hakuna makubaliano yoyote yaliyofikiwa na misaada katika ukanda wa Gaza iliyopitishwa ili kuwatoa raia wa kigeni nje ya eneo hilo.

Jeshi la Israel lilisema kuwa linawahamisha wakazi wa maka wake na Lebanon, kaskazini mwa Israel, wakiwamo wakazi katika vijiji 28 vilivyo umbali wa kilometa mbili kutoka katika mpaka huo.

Hatua hiyo imechukuliwa baada ya mashambulizi yaliyofanywa kati ya Israel na wanamgambo wa Hezbollah wa Lebanon na kusababisha kifo cha mtu mmoja. **DW**

## Msaada wahitajika ajali ya meli

**KINSHASA,** DRC

NAIBU Gavana wa Jimbo la Equateur, nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) Taylor Ng'anzi amesema wanahitaji msaada wa haraka kuwaokoa manusura, wa ajali ya meli iliyosababisha vifo vya zaidi ya watu 40.

Ajali hiyo ilitokea siku tatu zilizopita katika jimbo hilo lililoko kaskazini mashariki mwa DRC, ambako zaidi ya watu 100 walitoweka.

Pia alisema msaada huo utawawezesha kusaidia manusura ambao wamepoteza kila kitu na kurahisisha kurejea makwao. Na kwamba serikali ya mkoa wa Equateur pia inanuia kutoa huduma za kisaikolojia kwa watoto waliojeruhiwa ambao walipoteza wazazi wao wakati wa ajali hiyo.

Alisema juhudi za kuwatafuta manusura zinaendelea, akisema maiti iliopatikana hadi Jumapili jioni kwenye mto Kongo imezikwa mjini Mbandaka, mji mkuu wa jimbo hilo la Equateur.

Ngazi alisema kwa sasa wanaendelea na kutafuta pia familia za watu waliofariki pamoja na za manusura ili kurejesha baadhi ya bidhaa zilizookolewa kwenye meli hiyo.

Mashuhuda wamesema mashua hiyo ya HB Mapamboli iliosafiri kutoka Mbandaka kwenda Bolomba umbali wa kilomita mia moja halikufanikiwa kusonga mbele kutokana na uzito kupita kiasi, uliosababisha mashua hiyo kuzama dakika chache baada ya kuanza safari.

Viongozi wa Jimbo la Equateur wametangaza kuanzishwa kwa uchunguzi wa ajali hiyo. **DW**

# RICARDO AZITAKA 3 ZA YANGA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Singida Fountain Gate FC, Ricardo Ferreira, ameanza kupigia hesabu pointi tisa kwa mechi tatu za Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Yanga, Ihefu na Namungo.

Ferreira ambaye ameanza kazi rasmi jana ya kukinoa kikosi cha Singida Fountain Gate FC, amesema anahitaji pointi tisa dhidi ya Namungo FC Oktoba 21 na 26 dhidi ya Yanga kisha kubeba alama kama hizo atakapoivaa Ihefu FC Novemba Mosi, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana, Ricardo alisema licha ya kuwapo kwa muda mchache wa kufanya maandalizi kuelekea mechi dhidi ya Namungo FC, anahitaji kupata alama tatu katika mchezo huo na baadaye kwa Yanga ambayo watakuwa ugenini.

Alisema mechi ya mwisho ya kukamilisha pointi tisa ni dhidi ya Ihefu FC, ambayo watakuwa nyumbani, hivyo ni muhimu michezo yote kutafuta alama tatu ili kujiondoa katika presha za kuwapo chini ya msimamo wa ligi hiyo.

"Nilipata kuangalia baadhi ya mechi za timu ambazo tunatarajia kucheza nazo hivi karibuni, nimeona kikosi cha Singida Fountain Gate FC kuna wachezaji wazuri wa kuniwezesha kufikia malengo yangu," alisema Ricardo.

Aliongeza kwa falsafa zake na mbinu anazowapa wachezaji wake watafikia malengo yanayotarajiwa msimu ujao kuwa miongoni mwa timu nne ambazo zitashiriki michuano ya kimataifa.

Kikosi cha Singida Fountain Gate FC kimeweka kambi ya siku nne Mtwara na Ijumaa hii kitafunga safari kuelekea Lindi kukabiliana na wenyeji wao, Namungo FC, katika Uwanja wa Majaliwa, uliopo Ruangwa.




Mshindi wa 'Promotion' ya Maokoto Deilee kutoka SportPesa na tiGO Pesa akikabidhiwa mfano wa hundi ya Sh. milioni 15 na wachezaji wa Yanga, jijini Dar es Salaam wiki iliyopita. **PICHA: PIGAPICHA WETU**

## *Mshindi mil. 15/- Maokoto Deilee huyu hapa*

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI namba moja ya Michezo ya Kubashiri, SportPesa kwa kushirikiana na mtandao wa Tigo kupitia huduma ya TigoPesa zimewazawadia washindi wanne, ambapo wawili kati yao wamejishindia simu janja, huku Joseph Kabelwa akijishindia Sh. 1,000,000 na Diatus Ishengoma akitangazwa mshindi wa Sh. milioni 15, wa Kampeni ya'Maokoto Deilee'.

Promosheni hiyo ilizinduliwa Agosti 21, mwaka huu, ambapo iliwapa fursa watumiaji wa mtandao wa Tigo kuingia kwenye droo baada ya kuweka fedha zao kwenye akaunti zao za SportPesa, kupitia TigoPesa na kisha kuweka bashiri zao.

Akizungumza baada ya droo iliyochezeshwa Makao Makuu ya Ofisi ya SportPesa jijini Dar es Salaam wiki iliyopita, Ofisa wa Idara ya Uhusiano na Mawasiliano SportPesa, Lydia Solomon, alisema wamefanya droo yao ya mwisho ya Promotion ya Maokoto Deilee na mpaka wanahitimisha zaidi ya wateja 550 wamezawadiwa zawadi mbalimbali zikiwamo fedha na simu janja kabla ya kupatikana mshindi huyo wa jumla aliyeondoka na Sh. milioni 15.

"Tunapenda kuwashukuru wateja wetu wote walioshiriki promotion hii iliyodumu kwa siku 50, na huu ni mwanzo tu, sisi kama SportPesa tutaendelea kuwazawadia wateja wetu zawadi mbalimbali kwa kuendelea kushirikiana na Kampuni ya Tigo, na si Tigo peke yake hata mitandao mingine.

"Tunapenda kutoa rai kwa wateja wetu kuendelea kucheza na SportPesa ukiachana na promotion hii tuna bidhaa zetu zingine kama jackpot ya katikati ya wiki na Supa jackpot, ambapo huwa tunatoa washindi wa bonasi kila wiki," alisema Lydia.

Meneja Biashara wa TigoPesa, Fabian Felician, alisema kupitia promosheni hiyo ya Maokoto Deilee, wamefanikiwa kubadilisha maisha ya Watanzania wengi, kwani kuna ambao walikuwa hawana smartphone wameweze kupata huku wengine wakiongezea mitaji kwenye biashara zao.

## *Waendesha Baiskeli 'Twende Butiama' wapongezwa*

**Na Frank Monyo**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa, amepongeza juhudi za waendesha baiskeli wa msafara wa 'Twende Butiama', kwa kutimiza azma yao waliyojiwekea wakati wanaanza safari yao Dar es Salaam kwa kumuenzi Baba wa Taifa kwa vitendo kupitia utekelezaji wa shughuli za kielimu, afya na mazingira.

Waendesha Baiskeli hao walitumia siku 14, zaidi ya kilometa 1,500 kupita wilaya 20 za mikoa 10 tofauti nchini, kuhitimisha ziara yao iliyoanza Oktoba Mosi, mwaka huu jijini Dar es Salaam na kuwasili Mwitongo, Butiama jana Oktoba 14, ikiwa ni jitihada za kuenzi maisha na urithi aliotuachia Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Akizungumza wakati wa kupokea msafara huo nyumbani alikozaliwa Mwalimu Nyerere wilayani Butiama, Msigwa alipongeza juhudi hizo za kumuenzi Baba wa Taifa kwa vitendo kupitia utekelezaji wa shughuli za kielimu, afya, na mazingira.

"Nichukue fursa hii kuwapongeza waendesha baiskeli wa msafara wa Twende Butiama na uongozi mzima kwa ushujaa wa kipekee kuweza kufanikisha ziara hii. Waendesha baiskeli 75, wakiwamo wazee na watoto wameendesha siku 14, kilomita zaidi ya 1,500 kukatisha mikoa 10 na wilaya 20. Ni jambo la kujivunia na mnastahili pongezi za dhati na mfano wa kuigwa na jamii nzima. Lakini, cha kujivunia zaidi ni kwamba mliamua kutumia msafara huu wa baiskeli kumuenzi Baba wa Taifa," alisema.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa TEHAMA kutoka Kampuni ya simu za mkononi ya Vodacom Tanzania PLC, Athumani Mlinga, alisema: "Msafara wa Twende Butiama ni mfano wa kuigwa kwa ubunifu wao kwa kutumia zoezi la kuendesha baiskeli kutekeleza shughuli muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini."

## Aiyee afungua lango la 'hat-trick' Championship

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa zamani wa Mwadui FC, Salim Aiyee, amekuwa mchezaji wa kwanza kufunga mabao matatu katika mechi moja 'hat-trick' kwenye Ligi ya Championship msimu huu, akiiongoza Stand United kuiadhibu Ruvu Shooting mabao 5-0.

Ilikuwa ni mechi ya raundi ya sita ya ligi hiyo iliyochezwa juzi katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha.

Tayari mchezaji huyo ambaye alitamba Ligi Kuu msimu wa 2018/19 akipachika mabao 18 na kuwa wa pili kwenye orodha ya wafungaji bora nyuma ya aliyekuwa straika wa Simba, Meddie Kagere aliyepiga mabao 23, ana mabao manne kwenye mechi tano alizocheza mpaka sasa.

Mabao mengine ya Stand United yalifungwa na Masanja Jesto na Michael Mwinga, ambapo matokeo hayo yanaifanya Stand United kufikisha pointi saba, ikicheza mechi sita, ushindi mechi mbili, sare moja na kupoteza tatu, ikiwa kwenye nafasi ya 11 ya msimamo ambao unaongozwa na TMA yenye pointi 14.



## ZISIKUPITE

### SMITH ATAKIWA NEWCASTLE

KIUNGO wa kati wa Arsenal na England, Emile Smith Rowe mwenye umri wa miaka 23, ananyatiwa na klabu nyingine ya Ligi Kuu ya England, Newcastle United. ***(Mirror)***

### INTER KWA IHEANACHO

INTER Milan wanahusishwa na kiungo wa West Ham raia wa Czech, Tomas Soucek, mwenye umri wa miaka 28 na mshambuliaji wa Leicester City raia wa Nigeria, Kelechi Iheanacho, 27. ***(FC Inter News)***

### SOUCEK MKATABA MPYA

KLABU ya West Ham inatazamiwa kuimarisha mazungumzo ya mkataba mpya na Tomas Soucek, ambaye anatarajiwa kuwa mchezaji huru msimu ujao. ***(Football Insider)***

### AWINDWA BAYERN

CHELSEA iko tayari kumuuza mlinzi wa England, Trevoh Chalobah mwenye umri wa miaka 24, Januari mwakani huku mabingwa wa Ujerumani, Bayern Munich wakimtaka. ***(Fabrizio Romano, kupitia Goal)***

### MBAPPE KUONGEZEWA OFA

KLABU ya Paris St-Germain itatoa ofa ya mwisho ya kumwongezea mkataba mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 24 wiki ijayo. ***(Sport)***

### POYET ATOA NENO IRELAND

KOCHA wa Ugiriki, Gus Poyet, amesema angependa kuinoa Jamhuri ya Ireland wakati fulani, baada ya kuiongoza timu yake kushinda mara mbili dhidi ya Waireland hao kwenye mechi ya kufuzu kwa Euro 2024. ***(Irish Independent)***

### SANA KUIPA CITY HELA

KLABU ya Manchester City inaweza kupata zaidi ya pauni milioni nane kwa sababu ya kipengele cha kuuzwa iwapo Liverpool itamsajili winga wa Bayern Munich na Ujerumani, Leroy Sane, 27. ***(Mirror)***

### RATCLIFFE BADO UNITED

UWEKEZAJI wa asilimia 25 wa Jim Ratcliffe katika Klabu ya Manchester United bado haujakamilika na huenda mazungumzo yakachukuwa muda mrefu. ***(Independent)***

### BARCA, BAYERN KWA WIRTZ

KLABU ya Bayern Munich na Barcelona zote zinamtaka kiungo mshambuliaji wa Bayer Leverkusen na Ujerumani, Florian Wirtz, 20. ***(Mundo Deportivo)***

### MCTOMINAY SOKONI

KLABU ya Manchester United haina haraka ya kumuuza kiungo wa Scotland, Scott McTominay mwenye umri wa miaka 26, lakini watazingatia makubaliano kama bei itakuwa sawa. ***(90 min)***

### SOLSKJAER APOTEZEWA

KOCHA wa zamani wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, hatakuwa kocha mpya wa Charlotte FC baada ya rais wa timu hiyo, Joe LaBue, kuandika kwenye mtandao wa kijamii. ***(Manchester Evening News)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GAVI AIBEBA HISPANIA EURO 2024, HAALAND NJE

**OLSO,** Norway

HISPANIA imejihakikishia nafasi ya kufuzu kwa Euro 2024 baada ya bao la Gavi kipindi cha pili kutosha kuwalaza Norway 1-0 nyumbani kwao Jumapili na wataungana na wapinzani wao wa Kundi A Scotland, huku Uturuki kutoka Kundi D pia ikifuzu.

**Hispania na Scotland zote zimefanikiwa kutinga kwenye nafasi mbili za juu zikiwa na pointi 15 katika michezo sita, huku Norway wakiwa nafasi ya tatu kwa pointi 10 baada ya kucheza mchezo mmoja zaidi, huku Uturuki ikiifunga Latvia kwa mabao 4-0 na kujihakikishia nafasi ya kufuzu.**

Gavi alifunga bao pekee katika mchezo huo kwa Hispania, ambao waliwaliza Norway na nyota wao wa Manchester City, Erling Haaland, hivyo kutinga fainali zitakazofanyika nchini Ujerumani mwakani.

**Ni kazi ya timu nzima, kuanzia fowadi wa kwanza hadi mlinda mlango, hasa safu ya...**

"Nimefurahishwa sana na matokeo. Tulicheza vizuri na kuzaa matunda," alisema Gavi baada ya mechi hiyo.

"Tuko kwenye mbio nzuri ya ushindi. Norway ni timu ngumu, zaidi ya yote walikuwa nyumbani. Kwa hivyo tuna furaha."

Usiku wa baridi huko Oslo, Hispania ilitawala mpira, lakini walijitahidi kuharibu safu ya ulinzi ya wenyejii, na ilionekana kama VAR inaweza kuwazuia kukata tiketi yao ya Euro wakati Alvaro Morata alipofunga bao la kipindi cha kwanza na likakataliwa.

Mshambuliaji huyo wa Hispania alikuwa kivutio tena wakati Gavi alipofunga bao la kwanza dakika nne baada ya mapumziko na VAR ikalikubali.

Gavi aliongeza: "Nadhani ni kwa sababu ya Morata, ambaye alikuwa katika nafasi ya kuotea, sijui kama alikuwa au la, lakini walitoa bao na ninafurahia hilo."

"Ni kazi ya timu nzima, kuanzia fowadi wa kwanza hadi mlinda mlango, hasa safu ya ulinzi, mabeki wa kati walikuwa wa kustaajabisha," alisema kocha wa Hispania, Luis de la Fuente. "Lakini ilikuwa timu nzima, ulikuwa mchezo kamili.

"Unapokuwa na mtazamo na shauku unaweza kushinda dhidi ya yeyote. Hatari inaweza kuja kutokana na hali hizo na tulikabiliana nayo vema, dhidi ya timu yenye nguvu katika kipengele hicho cha mchezo."

Wao Uturuki walifuzu kwa michuano hiyo baada ya kuifunga Latvia wakiwa nyumbani.

# ONANA ATARUDI TENA INTER – MAROTTA



**MILAN,** Italia

MTENDAJI Mkuu wa Inter, Giuseppe Marotta, amekataa kuondoa uwezekano wa kurejea katika klabu hiyo, mlinda mlango wa Manchester United, Andre Onana.

Onana amekuwa chini ya shinikizo kubwa baada ya kuanza vibaya katika soka lake kule Old Trafford, na alifanya makosa dhidi ya Brentford katika ushindi mwembamba wa 2-1, pia akawa katika wakati mgumu dhidi ya Bayern Munich na Galatasaray kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, alijiunga na United akitokea Inter kwa mkataba wa karibu pauni milioni 50, akisaini mkataba wa miaka mitano kumrithi David de Gea kama namba moja wa muda mrefu wa 'Mashetani Wekundu' hao, lakini mambo yanaonekana kumwendea vibaya.

Mkataba wa Onana uliwakilisha biashara kubwa kwa Inter iliyo na uhaba wa fedha, ambao walimnunua bila malipo kutoka kwa wababe wa Uholanzi, Ajax miezi 12 tu iliyopita, na kuiruhusu klabu hiyo kuwekeza fedha katika kuwasajili Yann Sommer na Benjamin Pavard kutoka Bayern Munich.

Mkurugenzi Mtendaji wa Inter, Marotta aliliambia Gazzetta dello Sport (kupitia Daily Mail) kuhusu uwezekano wa kurejea San Siro: "Siwezi kutabiri siku zijazo, lakini katika soka lolote linaweza kutokea. Kwa hakika, ilikuwa hivyo.

"Pia ilikuwa mpango mzuri kumsajili bure na kuuzwa kwa fedha hizo."

Onana ametawala vichwa vya habari wiki za mwanzoni mwa msimu, huku uchezaji wake wa kutojali ukichangia hali mbaya ya United kwa ujumla.

Vijana wa Erik ten Hag tayari wamepoteza michezo minne ya Ligi Kuu England - na walihitaji bao la dakika za lala salama la Scott McTominay ili kuepuka maafa dhidi ya Brentford - na hawana pointi katika mechi zao mbili za Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kipa maarufu wa zamani wa United, Peter Schmeichel, hivi majuzi alifichua kwamba amekuwa akizungumza na Onana, akielezea ushauri ambao ametoa juu ya jinsi ya kusonga mbele kutokana na makosa.

"Ninajaribu kuzungumza naye kuhusu jinsi inavyokuwa Manchester United, kile unachopaswa kuchukua," alisema Mdenmark huyo.

"Chochote ulichokifanya ni lazima ukiweke kwenye boksi moja kwa moja na uweke pembeni. Kwa hiyo ukikosea kwenye mchezo, inaweza kuwa kosa tunaloliona, linaweza kuwa kosa ambalo hatufanyi."




# Ghana yamtaka Nketiah



**LONDON,** England

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa Ghana, Chris Huhton, hajakata tamaa kwenye matumaini ya kumshawishi mshambuliaji, Eddie Nketiah, aache kuichezea England na kuhamia Ghana.

Mshambuliaji Nketiah alizaliwa Lewisham, Kusini mwa London na alichezea timu nyingi za vijana za England na kuweka rekodi ya kuwa kinara wa mabao kwa timu ya chini ya miaka 21.

Lakini, wazazi wake ni Waghana, hivyo anakubalika kuichezea 'Black Stars' inayonolewa na Hughton.

Hughton mwenye umri wa miaka 64, alisema: "Baadhi ya wachezaji wamekuwa wazi kila wanachotaka kukifanya. Wengine hawana uhakika na wengine wanataka kuona mambo yanavyoendelea.

"Nafikiri kitu kama hiki kipo kwenye kesi ya Eddie. Hatuwezi kukata tamaa kumshawishi ili aje Ghana. Lakini, hilo linategemea na mchezaji kile ambacho anataka."

Hughton bado pia anapambana kuona kama Callum Hudson-Odoi naye atabadili utaifa wake, ambapo staa huyo wa Nottingham Forest mwenye umri wa miaka 22, ameshaitwa mara mara tatu kwenye kikosi cha England, lakini mara zote hizo ilikuwa 2019 kipindi hicho alipokuwa chini ya umri wa miaka 21, ambao kwa sasa si kikwazo akibadili utaifa.

## Serikali yaigeukia TFF kuita Stars kimya kimya

**Na Shufaa Lyimo**

SERIKALI imelitaka Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), lirudishe utaratibu wa awali wa kuwatangazia Watanzania wachezaji wanaoitwa Timu ya Taifa (Taifa Stars), ili waweze kuwafahamu pamoja kutoa maoni yao badala ya kufanya kimyakimya.

Hayo yamesemwa jana na Kaimu Mkurugenzi wa Maendeleo ya Michezo nchini, Ally Mayay Tembele, wakati akifanya mahojiano maalum na gazeti hili, lilipotaka kujua nini maoni ya serikali kuhusu utaratibu huo mpya wa TFF.

"Ninaaamini TFF italifanyia kazi suala hili ili warudishe ule utaratibu uliokuwapo mwanzo utakaowasaidia Watanzania kuifahamu timu yao ili wapate muda wa kumchambua mchezaji mmoja mmoja badala ya kushtukizwa kwa kuona tayari wako kambini," alisema Tembele.

Alisema Watanzania wana haki ya kujua kikosi chao hasa ukizingatia Rais wa Awamu ya Sita, Samia Suluhu Hassan, anazipambania kwa kiasi kikubwa timu za Taifa ili nchi ifike mbali kupitia michezo.

"Rais wetu anafanya jitihada kuhakikisha timu zetu za taifa zinafika mbali kwa kuamua kutoa fedha kwa timu itakayofanya vizuri ili kuwapa motisha wachezaji," alisema.

Katika hatua nyingine alikipongeza kikosi cha timu hiyo kwa kupata sare ya bao 1-1 dhidi ya Sudan katika mchezo wa kimataifa wa kirafiki uliochezwa Saudi Arabia juzi usiku.

## Robertinho: Nimeandaa 'supa sub' ya kuiua Al Ahly

INATOKA UKURASA 24

ya kufungwa mabao 5-0 jijini Cairo, 2021 zilikuwa tena kundi moja la Ligi ya Mabingwa Al Ahly ikifa tena kwa mara nyingine kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa bao 1-0 lililotiwa nyavuni na Miquissone ambaye baadaye alinunuliwa na timu hiyo, lakini kwa sasa amerejea tena Simba na atakuwapo Ijumaa.

Katika mechi ya marudiano nchini Misri 2020, Simba ilionesha ukomavu baada ya Al Ahly nayo kushinda kwa tabu bao 1-0.

# AMROUCHE AKUNA KICHWA TATIZO LA KIPA TAIFA STARS

**Na Saada Akida**

BAADA ya sare ya bao 1-1 kwenye mchezo wa kirafiki dhidi ya Sudan uliochezwa katika Uwanja wa King Fahd Altaif, nchini Saudi Arabia, Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Adel Amrouche, amesema ataifanyia kazi changamoto ya mapungufu ya golikipa kwenye kikosi chake.

Akizungumza baada ya mechi hiyo kumalizika, kocha huyo raia wa Algeria, alisema mechi hiyo ilikuwa kipimo kizuri, lakini kulikuwa na makosa ya ajabu yaliyojitokeza ikiwamo mawasiliano ya wachezaji wenyewe kwa wenyewe na kutoheshimu mchezo.

**"Tunahitaji kuyarekebisha haraka sana, changamoto ya kipa nafahamu Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), wanalifanyia kazi," alisema Amrouche.**

Beno Kakolanya alisimama langoni na kwa sasa amekuwa ndiye kaimu kipa namba moja baada ya kuumia kwa Aishi Manula ambaye kwa sasa amepona, Simba ikifikiria kutaka kumweka langoni katika mechi ya Ijumaa dhidi ya Al Ahly kwenye mechi ya ufunguzi ya African Football League, AFL.

Nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samata, alisema ni kipimo kizuri kwa mwalimu kuona kikosi chake na ndio maana ya mechi ya kirafiki kwa sababu wanaelekea kwenye mashindano, hivyo kocha anaangalia nini anakitaka na ni wachezaji wa aina wa gani anataka ili kuandaa jeshi lake.

"Wachezaji gani anataka, kuna kitu anataka kukiona kwani hakuna muda tena baada ya mchezo huu kuna michezo ya mashindano.

"Mwezi wa 11 na 12 tuna mechi za kufuzu, mwalimu anaangalia nini anaweza kufanya yeye atatoa tathmini yake nini ameona na ni aina gani ya kikosi anatarajia kuwa nacho," alisema Samata.

Naye Saimon Msuva, alisema haukuwa mchezo mwepesi sana kwa sababu Sudan ni timu nzuri na wanaiheshimu japokuwa matokeo yamekuwa sare ya bao 1-1, lakini pia wana maandalizi ya michezo ambayo iko mbele yao ya kujiandaa na AFCON.

"Kikubwa sasa hivi tunaangalia mashindano yaliyo mbele yetu ambayo kila Mtanzania anaangalia na ana kiu ya kuona timu yao ya taifa inafika mbali," alisema.

**MECHI NA SALA...**



Baadhi ya wachezaji wa Taifa Stars na benchi lake la ufundi, ambao baada ya mechi ya kirafiki dhidi ya Sudan iliyochezwa juzi nchini Saudi Arabia, walienda kufanya ibada katika Msikiti wa Makkah uliopo nchini humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Katwila anukia Mtibwa Sugar*

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuondoka Klabu ya Ihefu FC, Kocha Zuberi Katwila, huenda akajiunga na Mtibwa Sugar kuchukua nafasi ya Habib Kondo ambaye anaweza kubaki kama kocha msaidizi au kuondoka.

Habari zilizopatikana ndani ya vikao vya timu hiyo, zinaeleza wengi wamekubaliana kuwa Zuberi, straika wa zamani wa timu hiyo ndiye achukue mikoba ya kocha huyo, huku mwenyewe akibainisha kuwa baada ya wiki moja au mbili atarejea tena kuifundisha timu ya Ligi Kuu.

"Kuondoka kwangu Ihefu kulikuwa ni makubaliano ya pande zote mbili, hakukuwa na tofauti za misimamo au mtazamo, tulikaa na kukubaliana, huu ni mpira, nimeishi miaka mitatu na Ihefu, nilifika pale nikafundisha lakini timu ikashuka nikakaa nayo hadi ikapanda, nilipata ushirikiano mkubwa sana, nawashukuru viongozi wa Ihefu," alisema kocha huyo.

Alisema kwa sasa yupo kwenye mapumziko kidogo nayo ni ya kujadili na kukubaliana na ofa ambazo zipo mezani.

"Kwa sasa nina ofa nyingi nazifanyia kazi na siwezi kukaa sana zaidi ya wiki moja au mbili hivi, nitaonekana tena kwenye Ligi Kuu," alisema kocha huyo ambaye hadi anaondoka aliiongoza Ihefu kucheza mechi tano ikishinda mbili na kupoteza tatu, ikiwa nafasi ya nane kwa pointi sita.

Ofisa Habari wa Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru, alisema wiki hii watakuwa na kikao cha mwisho ambacho kitakuwa na maamuzi akikwepa kusema kama itamtangaza Katwila kuwa kocha wao.

"Vikao tumefanya wiki nzima na tunatarajia kufanya kikao cha mwisho ambacho ndicho kitatoa maamuzi ya nini kifanyike ili kuinusuru timu yetu ambayo haifanyi vizuri, nadhani kikao cha mwisho ndicho kitatoa taswira yote.

"Tulikuwa na mijadala kwa nini timu yetu haifanyi vizuri, kwa nini ipo nafasi ya 15, ikicheza mechi tano ikitoa sare mbili na kufungwa mechi tatu, nafikiri baada ya hapo watu wote watajua nini kimeamuliwa ili kuinusuru timu," alisema Kifaru.

Kwa upande wa Ihefu SC, tayari nafasi yake imechukuliwa na kocha wa zamani wa Simba, Moses Basena.

Michezo
Jumanne Oktoba 17, 2023
Nipashe



‘Onana atarudi tena Inter Milan’ UKURASA 22

# Robertinho: Nimeandaa ‘supa sub’ ya kuiua Al Ahly

●●● Asema anajua sasa wanamwita ‘Mr. Objective’, awataka waje uwanjani...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI wapinzani wao, Al Ahly ya Misri, wakitarajiwa kutua nchini leo tayari kwa mchezo wa ufunguzi wa African Football League, Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho Oliveira, amesema ameshakiandaa kikosi chake kwa ajili ya mechi hiyo itakayopigwa Ijumaa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa huku akitambia kuwa na ‘supa sub’ ya kuweza kubadili matokeo kipindi cha pili.

**Simba na Al Ahly Ijumaa watakata utepe katika michuano hiyo inayoshirikisha klabu nane bora barani Afrika, zingine zikiwa ni Wydad Casablanca (Morocco), Mamelodi Sundowns (Afrika Kusini), Esperance Tunis (Tunisia), Petro Atletico de Luanda (Angola), Enyimba FC (Nigeria) na TP Mazembe (DR Congo).**

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Robertinho alisema kikosi chake kiko tayari kuwavaa Mabingwa wa Afrika, lakini yeye kama mwalimu ni lazima achague nani wa kuanza na kwa sababu gani, lakini ana kazi ya kuchagua wale ambao watasubiri ili kuingia kipindi cha pili kwa ajili ya kubadilisha mbinu, kusaidia wenzao watakapokuwa wamechoka au tatizo lolote litakalijitokeza.

“Kila kitu kiko tayari hapa kilichobaki ni kuchagua nani wa kuanza, kikosi gani nianze nacho na wachezaji gani wa kukaa benchi kwa ajili ya kusubiri wenzake, kwa mfano kwa sasa ninaye mchezaji wangu ambaye namtegemea sana akiingia kipindi cha pili na anabadilisha mchezo, Luis (Miquissone), unajua aliumia, kwangu mimi ni muhimu sana.

“Natarajia tutakuwa na mechi ngumu, lakini tumejiandaa, siku zote mpira si jambo la siri, tumejiandaa kucheza vizuri na kushinda ndiyo malengo yetu, nimeona watu wengi hawasemi tena jina langu ni Robertinho badala yake wananiita Mr. Objective na wataona siku hiyo waje kwa wingi uwanjani,” alisema kocha huyo raia wa Brazil.

Simba inakwenda kucheza na Al Ahly kwenye ufunguzi wa michuano hiyo ikiwa na rekodi ya kuifunga kwenye mechi zote tatu ambazo imewahi kukutana nayo hapa nchini, lakini hushindwa kufanya hivyo ikiwa ugenini.

Hata hivyo, Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, ambaye jana kwa kushirikiana na wanachama na mashabiki wa timu hiyo walikuwa na kazi moja tu ya kuipamba Dar es Salaam kwa mabango kuelekea mechi hiyo ya ufunguzi, amesema kwa sasa Simba kuifunga Al Ahly siyo stori tena, badala yake safari hii wanataka kuiondosha kwenye mashindano.

Mara ya kwanza zilikutana mwaka 1984 kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza kwenye Kombe la Washindi barani Afrika (sasa Kombe la Shirikisho), Simba ikishinda mabao 2-1, yaliyowekwa kwenye kamba na Zamoyoni Mogella na Mtemi Ramadhani, lakini ikaenda kutolewa Cairo nchini Misri kwa kufungwa mabao 2-0.

Zilikutana tena Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi 2019, Simba ikishinda bao 1-0 la Meddie Kagere, na hii ni baada

INAENDELEA UKURASA 23

## BADO SIKU 3!...



Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, akiongoza na mashabiki wa klabu hiyo kupamba kwa mabango vyombo vya usafiri na sehemu mbalimbali jijini Dar es Salaam jana, kuelekea mechi ya ufunguzi ya African Football League Ijumaa wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Gamondi sasa awageukia kina Bacca, Mwamnyeto

**Na Saada Akida**

KUELEKEA mechi dhidi ya Azam FC, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema anaifungia kazi safu yake ya ulinzi inayoongozwa na Bakari Mwamnyeto, Ibrahim Bacca na Dickson Job akitaka kuepuka yasitokee kama yaliyowakuta dhidi ya Ihefu FC mwanzoni mwa mwezi huu.

Yanga itakipiga dhidi ya Azam FC, Jumamosi wiki hii kwenye mechi ya raundi ya sita ya Ligi Kuu Tanzania Bara, huku kocha huyo akiwa na kumbukumbu ya timu yake kuruhusu mabao mawili kwenye mechi moja wakati wakikubali kipigo cha 2-1 dhidi ya Ihefu FC, Oktoba 4, mwaka huu katika Uwanja wa Highland Estate, Mbarali mkoani Mbeya.

Akizungumza na Nipashe jana, Gamondi alisema mikakati yake mikubwa pamoja na kikosi chake ni kuona pamoja na ukali wa kutosha wa Azam FC, ni kuhakikisha wanafunga mabao mengi kwenye mchezo huo, lakini kutoruhusu kufungwa ovyo.

“Najua kuwa hautokuwa mchezo mwepesi kwa sababu wanatujua na sisi tunawajua vema, ukiangalia ina wachezaji ambao walishacheza hapa kwetu na hilo nimeona wakati ule Tanga kwa sababu wachezaji wote walionesha kukamiana kutokana na kila timu kujua mpinzani wake.

“Lakini kazi kubwa ni kuona tunafanikiwa kuharibu rekodi yao kwa kuona tunafunga mabao ya kutosha kwa sababu kama timu tunataka kuona tunasogea kutoka katika nafasi ambayo tupo nayo kwa sasa, “ alisema Gamondi.

Alisema kwa timu kubwa kama Yanga si kitu kizuri timu iwe inaruhusu mabao mara kwa mara, na hasa mawili kwenye mechi moja, akisema hataki tena hilo litokee.

Kwa sasa Yanga inajiandaa na mechi hiyo ikiwa kwenye nafasi ya tatu kwa pointi 12, huku Azam ikiwa nafasi ya pili na pointi zake 13, zote zikicheza mechi tano, huku kileleni ikitawala Simba iliyopata matokeo kwa asilimia 100 kwenye michezo yake mitano.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042